Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumapili Julai 21, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0581744
www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
JUMAPILI
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com

UKURASA WA 2
**DC**, OCD waingia matatani madai ya kuzuia amri ya mahakama

UKURASA WA 2
**Majaliwa** ataka elimu utambuzi kwa wasio raia



UKURASA WA 3
**Ajali** basi, Hiace yaua M/kiti UWT, yajeruhi 12




MORATA ATUA RASMI
UKURASA 21



# Utata tril. 1.7/- kutolewa BoT

UKURASA 4

RIPOTI MAALUMU - 2
## Wanasaikolojia tiba waonya kamari, shisha kwa watoto
UKURASA 5



## Rais Samia atoa kauli utekaji, mauaji watoto
UKURASA 3

MICHEZO SIMBA SC YAKIRI DILI LA MPANZU GUMU UK.24
KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Majaliwa ataka elimu utambuzi wasio raia

**Adela Madyane,** KIGOMA

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amelitaka Jeshi la Uhamiaji kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuwatambua na kutoa taarifa za watu ambao si raia wa Tanzania katika kila kituo cha uandikishaji.

Aliyasema hayo jana katika uzinduzi wa kuboresha daftari la kudumu la wapigakura uliofanyika katika viwanja vya Kawawa vilivyoko Manispaa ya Kigoma Ujiji.

Alisema mwananchi ndiye mtu wa kwanza kutambua nani ni mtanzania na nani si mtanzania katika maeneo wanamoishi.

Majaliwa aliagiza kuwapo ushirikiano baina yao ili kutambua wasio na sifa ya utanzania hawajiandikishi katika daftari hilo na kufanya mchakato huo kufanyika kwa ufanisi mkubwa.

"Watanzania lazima tuwe wazalendo, upigaji kura ni kwa sisi watanzania, tunachagua viongozi watakaoliongoza taifa. Tunachagua viongozi ambao watakuja kuwa viongozi wa mitaa yetu na vitongoji vyetu, kwanini kuruhusu mtu wa nje aje atupigie kura?

"Atatuamlia ambavyo sisi hatutaki, kwahiyo tusiruhusu mtu yeyote kutoka nje ajiandikishe katika daftari la mpigakura" aliagiza.

Majaliwa alisema kila mtanzania asimamie mchakato huo kwa uadilifu, kwa kutoa taarifa sahihi za raia anayetaka kujiandikisha ambaye si mtanzania.

Aliwataka viongozi wa vyama vya siasa kuweka mawakala watakaosimamia mchakato huo kutoka katika kijiji husika kwakuwa ndio wanaowafahamu wananchi wa maeneo yao, na hivyo kuwa rahisi kutambua ambao hawana sifa za kuandikishwa kama raia wa Tanzania.

"Ninaomba mawakala wote muwe wazalendo na makini kuangalia kila anayekuja kuboresha taarifa zake na kufuatilia namna anavyohojiwa, kwakuwa maelezo yake yanaweza kutusaidia kutambua aliye raia na asiye raia," alisema.

Majaliwa aliwataka watendaji na wote watakaohusika katika mchakato huo kutumia lugha nzuri na kutekeleza wajibu huo kwa kuzingatia sheria na taratibu zinazotolewa na tume na kuhakikisha unakamilika bila kuwa na dosari yoyote.

Kwa upande wa asasi zilizopata vibali vya kutoa elimu, Waziri mkuu Majaliwa alisema zinapaswa kutoa elimu sawasawa na makubaliano yaliyowekwa katika mwongozo na kwamba, wasivunje sheria nyingine za nchi kwa kigezo cha kuwa na kibali cha kutoa elimu.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Ndariananga, alisema mchakato huo umeshirikisha wadau mbalimbali wa uchaguzi ikiwa ni utekelezaji wa falsafa ya 4R ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Akitoa taarifa ya Tume Huru ya Uchaguzi, Mwenyekiti wake, Jacobs Mwambegele, alisema mchakato wa kuboresha au kuhamisha taarifa kwa njia ya kieletroniki umeboreshwa katika simu zote.

Jaji Mwambegele alisema asasi 157 zimepewa vibali vya kutoa elimu hiyo huku asasi nyingine 33 za ndani na nane za kimataifa zikipewa vibali vya kuwa waangalizi wa uandikishaji kwa ajili ya kutazama uendeshaji wa mchakato huo.

Alisema taasisi hizo zilizopewa vibali zimepewa nyaraka mbalimbali ikiwamo Katiba, sheria na miongozo inayosimamia jukumu la utoaji elimu ya mpigakura na utazamaji.




Mitambo ya kunyanyua vitu vizito ikinyanyua nguzo za taa za kuongozea gari katika barabara ya Kawawa Ilala jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# DC, OCD matatani madai ya kuzuia amri ya mahakama

**Na Benny Kingson,** TABORA

Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Deusdedit Katwale na Kaimu Mkuu wa Polisi Wilaya (OCD), Seleman Mwampamba, wameingia matatani baada ya kudaiwa kuzuia utekelezaji wa amri ya mahakama.

Kutokana na madai hayo, viongozi hao ambao wanahusika pia na masuala ya ulinzi na usalama katika wilaya, wanatarajiwa kupandishwa kizimbani Agosti 28, mwaka huu, katika Mahakama Kuu Kanda ya Tabora.

Hatua hiyo inatokana na madai ya Juma Nombo (70) na Mohamed Nombo (68), wakazi wa Dar es salaam kwamba Katwale na Mwampamba wamezuia utekelezaji wa amri ya mahakama.

Walisema juzi kwamba Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Tabora, lilitoa hukumu na amri kupitia shauri la maombi madogo Na. 15 la mwaka 2014 kati ya marehemu mama yao mzazi, Asha Shabani, ambaye alikuwa mwombaji dhidi ya Kasawa Willa ambaye ni mjibu maombi.

Kwa mujibu wa wazee hao, Katwale anadaiwa ndiye aliyemwagiza OCD kutokutoa askari kwenda kusimamia utekelezaji wa amri iliyotolewa na mhimili huo wa serikali unaosimamia sheria na haki.

"Tunashangaa viongozi hawa ambao wamepewa dhamana ya kuongoza,kulinda amani na kusimamia haki,wanajua sheria na kufahamu mipaka ya kazi zao pia wanatambua kuwa uamuzi wa mahakama huwa hauingiliwi. Tunasikitika sana kufanyiwa haya na kusumbuliwa," walisema.

Juma ambaye ni msimamizi wa mirathi ya marehemu mama yao huyo aliyefariki dunia Julai 17, 2017 Mahakama hiyo ilimpa ushindi Machi 21, 2024 na Mkasiwa Auction Mart ambaye ni dalali wa mahakama, alipewa amri ya kumwondoa Willa kupitia barua yenye kumb. Na.TBR/LHT/Misc. Land Appl. Na.15/2024.

"Dalali alitoa notisi kwa Willa ya siku 14 kuondoa mali zake katika eneo letu lenye ekari 60 lililopo Kidatu Kata ya Mtendeni na OCD alipewa taarifa hiyo na kutakiwa kutoa askari wa kusimamia utekelezaji wa amri hiyo lakini alidai amepewa maagizo na DC kutotoa askari hadi atakapokutana na pande zote mbili zenye mgogoro," alisema.

Alisema dalali huyo alitoa taarifa ya utekelezaji kazi kwa mahakama Mei 15, 2024 kupitia barua yenye kumb.Na.MAM,MAOMBI MADOGO Na.15/2014 akieleza yaliyotokea kwa OCD kuhusu agizo alilopewa na mkuu huyo wa wilaya.

Juma alisema Machi 23, 2024 alipigiwa simu na OCD kwamba wanahitajika kwa mkuu wa wilaya na walifika na kumuonyesha nyaraka zote lakini kiongozi huyo alidai atasikiliza pande zote mbili na kutoa uamuzi kitu ambacho hawakuafikiana naye.

Naye Mohamed alisema walikwenda kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Richard Abwao, wakamweleza suala lao na kamanda huyo alimwagiza OCD kushughulikia suala hilo kupitia barua ya Mei 20, 2024 yenye kumb.Na.GB.536/379/01/36.

"Tuliwasiliana pia na (Mkuu wa Jeshi la Polisi) IGP Camilius Wambura kipindi akiwa Tabora na kumweleza shida yetu na aliahidi kulifanyia kazi na tulimwandikia Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha, kumweleza kero yetu kupitia barua ya Mei 16, 2024 yenye kumb. Na.JK/TBR/3/2024 na nakala tukaituma Ikulu kwa Rais (Samia Suluhu Hassan),"alisema.

Alisema baada ya barua hiyo, mkuu huyo wa mkoa aliwakutanisha na mkuu wa wilaya na alimwuliza kinachoendelea kuhusu suala lao na kujibu kuwa analishughulikia lakini akadai alitoa kauli ya kejeli kwamba kama wameshindwa maisha warejee kwao Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa waraka ulitolewa na aliyekuwa Jaji Kiongozi Eliezer Feleshi kupitia barua ya Septemba 30, 2020 yenye kumb.Na. CHA.26/228/01/37, viongozi walielekezwa kuhusu vitendo vya kuingilia na kuzuia utekelezaji wa amri na tuzo za mahakama huku akihimiza uamuzi wa mhimili huo wa dola kuheshimiwa.

Katwale alipotafutwa kutoa ufafanuzi kuhusu tuhuma hizo na kwamba anakwepa kupokea wito wa kuitwa mahakamani hakupatikana ofisini kwake kwa maelezo kuwa anaumwa. Hata alipopigiwa simu hakupokea na alipotumiwa ujumbe mfupi, awali alijibu yuko safarini na alipotumiwa ujumbe unaoeleza tuhuma hizo, hakujibu wala kutoa ushirikiano.

Kesi hiyo dhidi ya mkuu wa wilaya ya OCD yenye jalada namba 15946/2024 imepangwa kusikilizwa katika Mahakama Kuu Kanda ya Tabora chini ya Jaji Mfawidhi, Adam Mambi.

## HABARI KITAIFA

# Samia atoa kauli utekaji, mauaji watoto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema serikali isitupiwe lawama kutokana na vitendo vya utekaji na mauaji ya watoto vinavyoendelea hivi sasa nchini bali jamii inapaswa kuwajibika ili kukomesha hali hiyo.

Amesema jamii inapaswa kuwajibika ili kukomesha hali hiyo, huku akiwaomba machifu kuyakemea katika maeneo yao kwa sababu yanachafua taswira ya taifa.

Aliyasema hayo jana Ikulu ya Chamwino, jijini hapa wakati akizungumza na viongozi wa kimila pamoja na machifu kutoka mikoa yote nchini.

Rais alisema vitendo vya utekaji na mauaji ya Watoto, wakiwamo wenye ualbino, hivi sasa vimeibuka kwa wingi katika maeneo mengi nchini hali ambayo inapaswa kukemewa na kuchukuliwa hatua kali.

"Hivi sasa vitendo vya utekaji pamoja na mauaji ya watoto vimekuwa vikiripotiwa kila siku na namna vinavyoripotiwa serikali ndiyo inalaumiwa sana wakati kule yanakotokea mambo haya viongozi wa mitaa wapo, lakini hata machifu wapo wamekaa kimya.

"Nawaombeni mwende mkayakemee mambo haya, kwani yanatokea huko kwenye jamii zetu na yanachafua taswira ya taifa letu lenye sifa nje. Leo hii watu wakisikia mtu katekwa ama mtoto kuuwawa siyo picha nzuri.

"Mambo ya mauaji ya wenye ualbino yalishapotea kabisa, lakini sasa yanarudi kwa kasi na ukiuliza watu wanadai ni uchaguzi, lakini uongozi anatoa Mungu siyo kwa kuuwa mtu," alisema Samia.

Rais Samia aliwataka machifu wote nchini kusimamia mila na desturi za nchi na kupinga vitendo ambavyo vinaharibu utamaduni wa mtanzania.

"Maendeleo hayakwepeki lakini sasa lazima kama taifa tuzingatie mila na desturi zetu, tusifanye mambo ambayo ni kinyume na tamaduni zetu," alionya.

Rais Samia aliagiza machifu kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia katiba na sheria za nchi ili kuondokana na tabia ya kutoa adhabu ambazo zinavunja haki za binadamu na kudhalilisha utu wa mtu.

"Lakini pia mkatatue migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo imekuwa ikisababisha mauaji ya watu na kuleta uhasama miongoni mwa wanajamii na mara nyingi wakulima ndiyo wanaoonewa.

"Mimi mwenyewe kuna kipindi nilikuwa ninalima mpunga kule Morogoro, kuna wakati mpunga ulistawi hadi nikasema umaskini sasa basi, lakini siku moja tu mfugaji aliingiza mifugo yake (shambani) ndani ya dakika kumi tu, hakuna kilichobaki na nilipompeleka polisi, anajibu kwa dharau tu, eti 'ng'ombe kala majani siyo mpunga' "alisema.

Rais alimwagiza Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, kuharakisha mchakato wa uandaaji wa mwongozo utakaotumika kuwatambua na kuwasimamia machifu kutekeleza majukumu yao. "Nikutake Waziri Ndumbaro huu mwongozo muuharakishe ili tupate kitu ambacho kitawatambua na kuwasimamia machifu, vinginevyo tukiacha kila mtu afanye anavyotaka tutarudi kule ambako kutakuwa na uvunjifu wa katiba,"alisema.

# Ajali basi, Hiace yaua m/kiti UWT

**Na Halima Ikunji,** IGUNGA

WATU wawili, akiwemo Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Wilaya ya Igunga, Zawadi William (60), wamefariki dunia huku wengine 12 wakijeruhiwa kutokana na ajali ya basi kubwa na ndogo.

Ajali hiyo ilihusisha basi la kampuni ya MUMUKI lililokuwa likitoka Mpanda kwenda Arusha kugongana uso kwa uso na gari dogo aina ya Toyota Hiace.

Wakisimulia ajali hiyo iliyotokea katika kata ya Nanga, mashuhuda akiwamo Juma Iddy, walitaja chanzo cha ajali hiyo kuwa ni dereva wa basi kuwa mwendokasi bila kuchukua tahadhari licha ya kwamba ni la mkusanyiko wa watu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Richard Abwao, alisema ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 7: 00 mchana na kuwa ilisababishwa na dereva Richard Gabriel (42) aliyekuwa akiendesha basi lenye namba za usajili T 702 DJF aina ya HIGER.

Alisema baada ya kufika Nanga wilayani Igunga, dereva huyo alifanya uzembe wa kutaka kuyapisha magari mengine matatu na kukutana uso kwa uso na gari dogo aina ya Toyota Hiace lenye namba za usajili T 202 DHU.

Kamanda Abwao alisema tayari dereva huyo anashikiliwa na jeshi hilo kwa tuhuma za kutokuzingatia sheria za barabarani na kusababisha ajali na vifo.

Akithibitisha kupokea miili ya marehemu na majeruhi hao 12, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Igunga, Dk. Mirichades Magongo, alisema waliofariki dunia ni Zawadi Wiliam (60) na Kaseko Makami (40) wote wakazi wa wilayani hapa.

Aliwataja majeruhi waliowapokea kuwa ni Theresia Masali (24), Kamwa Jilili (65), George Ndalu mkazi wa Dodoma, Batholomao John (26) mkazi wa Igogo, Mary Joseph (37), Mary Sesu mtoto wa miaka miwili.

Wengine ni Wilfred Kingu (28), Pendo Ngusa (58), Christopher Bizimana (35), Allen Joseph na Maria Ndelege (45) huku kati yao, wanne walipatiwa rufani kwenda Hospitali ya Misheni ya Nkinga kutokana na kuvunjika baadhi ya viungo.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Utata Tril 1.7/- kutolewa BoT

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA



Gavana wa Benki Kuu, Emmanuel Tutuba. **PICHA : MTANDAO**

SHILINGI trilioni 1.7 zilizotolewa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na kutumiwa na serikali zimezua utata, mwandishi wa Nipashe Jumapili anaripoti.

Uchambuzi wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2022/23 uliofanywa na Taasisi ya WAJIBU umebaini utata huo.

Akiwasilisha ripoti za uwajibikaji 2022/23 zilizotokana na uchambuzi wa Ripoti za CAG uliofanywa na Taasisi ya WAJIBU, Meneja Programu za Utafiti na Miradi, Moses Kimaro, alisema jijini Dodoma mwanzoni mwa wiki kuwa katika mwaka huo wa fedha, serikali iliidhinishiwa na Bunge kukusanya na kutumia Sh. trilioni 41.48.

Hata hivyo, Kimaro alisema Taasisi ya WAJIBU imebaini kuwa ukaguzi wa CAG kuhusu Hesabu za Serikali Kuu kwa mwaka 2022/23, umebaini serikali ilikusanya Sh. trilioni 41.88, kukiwa na ziada ya Sh. bilioni 400.

Hata hivyo, makusanyo yaliyopelekwa Mfuko Mkuu ni Sh. trilioni 38.447. Sh. trilioni 3.433 hazikupita Mfuko Mkuu wa Serikali.

Uchambuzi umebaini kuwa serikali licha ya kukusanya trilioni 38.447 zilizopita Mfuko Mkuu, BoT iliipa (serikali) Sh. trilioni 40.18, hivyo Benki Kuu kuipa serikali Sh. trilioni 1.7 za ziada.

Vilevile, imebainika kuwa kati ya Sh. trilioni 3.433 ambazo hazikupita Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mwaka huo wa fedha, Sh. trilioni 3.197 zilipelekwa moja kwa moja kwenye miradi.

Benny Mwaipaja, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Wizara ya Fedha, alipotafutwa na Nipashe Jumapili Jumanne ya juma hili kuzungumzia utata huo, aliahidi kutafuta majibu kutoka kwa wataalamu wa wizara.

Hata hivyo, tangu siku hiyo hadi tunaingia mtamboni, Mwaibaja hakutoa majibu kuhusu utata huo licha ya kukumbushwa Jumatano saa 8:12 mchana, Alhamisi 3:21 asubuhi na jana saa 7:49 mchana.

**KUTOKA KWA CAG**

Iliporejewa Ripoti ya CAG kwa Mwaka 2022/23 kuhusu suala hilo, inaonesha kuwa katika mwaka huo wa fedha, serikali ilikusanya Sh. trilioni 41.880 ikiwa ni zaidi ya bajeti ya Sh. trilioni 41.480 kwa Sh. bilioni 400.

Kulinganishwa na Sh. trilioni 38.298 zilizokusanywa mwaka 2021/22, CAG anaripoti kuwa alibaini ongezeko la asilimia tisa sawa na Sh. trilioni 3.582.

Tathmini ya CAG kuhusu mwenendo wa makusanyo katika kila chanzo kwa mwaka 2022/23 inaonesha makusanyo ya kodi Tanzania Bara yalikuwa Sh. trilioni 22.583 sawa na asilimia 95.5 ya lengo la kukusanya Sh. trilioni 23.652, hivyo serikali haikukusanya Sh. bilioni 1.069.

Kwa mwaka 2021/22, makusanyo hayo yalikuwa Sh. trilioni 20.945, hivyo kuwapo ongezeko la makusanyo kwa Sh. trilioni 1.638 sawa na asilimia nane.

CAG anatipoti kuwa mapato yasiyotokana na kodi yaliyokusanywa na wizara, idara na sekretarieti za mikoa na taasisi nyinginezo yalikuwa Sh. trilioni 2.7095 sawa na asilimia 81 ya lengo la kukusanya Sh. trilioni 3.352, hivyo Sh. bilioni 643 hazikukusanywa. Kwa mwaka 2021/22, makusanyo ya eneo hilo yalikuwa Sh. trilioni 2.709 ya mwaka 2021/22, hivyo CAG amebaini ongezeko dogo.

Kwa upande wa makusanyo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa mwaka 2022/23, CAG anasema walikusanya Sh. trilioni 1.222 ikiwa ni zaidi ya lengo la kukusanya Sh. trilioni 1.012 (asilimia 21) sawa na ongezeko la Sh. bilioni 21.

Kulinganisha na makusanyo ya Serikali za Mitaa ya Sh. bilioni 892 ya mwaka 2021/22, CAG anasema alibaini ongezeko la Sh. bilioni 330 sawa na asilimia 37.

Upande wa misaada, katika mwaka wa fedha 2022/23, CAG amebaini misaada iliyopokewa ni Sh. bilioni 759 sawa na asilimia 69 ya lengo la kusaidiwa Sh. trilioni 1.101, hivyo kiasi cha Sh. bilioni 342 hakikukusanywa.

Kulinganishwa na misaada ya Sh. trilioni 1.305 iliyopokewa mwaka 2021/22, CAG anasema amebaini kupungua kwa misaada kiasi cha Sh. bilioni 546 sawa na asilimia 42.

CAG anasema kuwa mikopo ya ndani, makusanyo yake yanayotokana na mikopo ankara za hazina, hati fungani na ufadhili wa ndani, kwa mwaka 2022/23 yalikuwa Sh. trilioni 6.124 ikiwa ni zaidi ya bajeti ya Sh. trilioni 5.780 sawa na ongezeko la Sh. bilioni 344 (asilimia sita).

Kulinganisha na mikopo ya Sh. trilioni 6.489 zilizokusanywa mwaka 2021/22, CAG amebaini kupungua kwa mikopo ya ndani ya Sh. bilioni 365 sawa na asilimia sita.

Kwa upande wa mikopo ya nje yenye masharti nafuu, CAG anasema Sh. trilioni 5.523 zilipokewa katika mwaka wa fedha 2022/23 ikiwa ni zaidi ya lengo la kukopa Sh. trilioni 3.547 (Sh. trilioni 1.976 zikizidi sawa na ongezeko la asilimia 56).

Kulinganisha na mikopo ya Sh. trilioni 4.149 zilizopokewa mwaka 2021/22, hivyo CAG amebaini ongezeko la mikopo ya nje yenye masharti nafuu kwa Sh. trilioni 1.374 sawa na ongezeko la asilimia 33.

CAG pia anasema kwa upande wa mikopo ya nje isiyo ya masharti nafuu, Sh. trilioni 2.959 zilipokewa sawa na asilimia 97 ya lengo la kukopa Sh. trilioni 3.034, hivyo mikopo isiyo ya masharti nafuu ya Sh. bilioni 75 haikupokewa.

Mdhibiti anasema: "Mikopo isiyo na masharti nafuu imeongezeka kwa asilimia 64 au Sh. trilioni 1.150 kulinganishwa na Sh. trilioni 1.809 zilizopokewa mwaka 2021/22."

**MATUMIZI**

CAG anafafanua kuwa kati ya Sh. trilioni 41.880 zilizokusanywa, Sh. trilioni 38.447 zilipokewa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, hivyo kuwapo tofauti ya Sh. trilioni 3.4334.

Anasema tofauti hiyo inatokana na Sh. trilioni 3.656 zilizopelekwa moja kwa moja kwenye miradi kutoka kwa wadau wa maendeleo na makusanyo yaliyopelekwa Zanzibar ambayo hayapitii Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali pamoja na Sh. bilioni 223 zinazotokana na bakaa za makusanyo ya kodi za mwaka uliopita na makusanyo mengine yaliyopokewa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali nje ya makisio ya bajeti.

"Jumla ya matumizi yaliyofanywa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ili kugharamia matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/23 yalikuwa Sh. trilioni 39.523 bila kujumuisha Sh. bilioni 665.80 zilizotolewa kama fedha zilizorejeshwa (refunds) na matumizi mengine kwenye jumla ya makusanyo ya Sh. trilioni 38.447, hivyo kusababisha nakisi katika Benki Kuu (BoT) ya Sh. trilioni 1.742 kufikia tarehe 30 Juni 2023," CAG anafafanua.

**RIPOTI MAALUMU - 2**

# Wanasaikolojia tiba waonya hatari kamari, uvutaji shisha kwa watoto

**Na Romana Mallya**

HII ni sehemu ya pili ya ripoti hii inayoangazia kushamiri kwa kamari na uvutaji wa shisha katika makazi ya wananchi kunakohusisha watoto. Katika sehemu ya kwanza jana, kulikuwa na ushuhuda wa namna vitendo hivyo vilivyoenea Kinondoni mkoani Dar es Salaam, hususani eneo la Mwananyamala. Katika sehemu hii ya pili, wasaikolojia tiba wanaeleza kwa undani athari za kiafya wanaocheza kamari na wanaovuta shisha, huku mamlaka za kiserikali zikianika hatua inazochukua kuthibiti vitendo hivyo. Sasa endelea...

Elizabert Mbuya, mfanyabiashara wa mgahawa ulioko eneo la Kabanakabana, Mwananyamala, anayechezesha pia kamari katika makazi ya watu, anakiri amekuwa akipokea watoto wa jirani wakitaka kucheza.

Mbuya anasema watoto hao wanapofika, huwafukuza na wakati mwingine kwa wale ambao wazazi wao anawafahamu huwajulisha.

"Hapa nina mgahawa kama unavyoona ninauza supu na chapati, lakini ninafanya biashara huko ndani ya kuuza bia na nina mashine hii ya kamari. Sijaweka tangazo la mtoto haruhusiwi.

"Ni kweli watoto huwa wanakuja hapa na fedha mfano Sh. 200 kutaka kucheza na hii ni kwa sababu biashara yangu iko katikati ya makazi ya watu ila huwa siwaruhusu," anasema.

Siku nne tangu kutolewe maagizo na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla, kuhusu kero hizo zilizotolewa na wananchi, jana Nipashe ilishuhudia baadhi ya maeneo michezo hiyo imeondolewa, huku shisha ikidaiwa kuuzwa usiku mnene.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Sindano, Kata ya Makumbusho, Kinondoni, Selemani Mohamed, akizungumza na mwandishi wa habari hii jana ofisini kwake, alisema wameanza kufanyia kazi maagizo ya Makalla aliyotoa Julai 17, mwaka huu.

Alisema tayari wenyeviti wa mitaa sita ya Kisiwani, Kichangani, Minazini, Mbuyuni na Makumbusho na wake, wameitwa na Mtendaji wa Kata na diwani na kukubaliana kukutana kesho (Jumatatu) kujadili hatua za kuchukua baada ya maagizo kutolewa.

"Juzi (Julai 18) katika mtaa wangu tulikuta mashine za kamari kama 11, kati ya hizo, tano ziko kwenye vyumba na zingine nje ya nyumba kwenye makazi ya watu. Tunatoa elimu hatutaki kuona watoto huko wakicheza kamari baadhi wamezificha," alisema.



Dk. Peter Mfisi.



Catherine Lamwai

Mohamed alisema katika mtaa wake tatizo kubwa ni kamari ambazo baadhi ya wahusika walioko mtaani wamekutwa wana nyaraka za kufungua biashara hizo kutoka manispaa husika (Kinondoni), hivyo kupitia kikao kitakachofanyika kitaamua nini kifanyike.

"Unaponiambia mimi mtu wa chini nichukue hatua kidogo unanipa mtihani, ndio maana nimeshukuru tulivyosikia kesho kutwa (Jumatatu) kutakuwa na kikao ambacho kitajumuisha diwani, Mtendaji Kata na polisi kata naamini utatoka uamuzi utakaolingana na maelekezo yaliyotolewa awali," alisema.

### WATAALAMU WAONYA

Msaikolojia Tiba kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Isaac Lema, anasema sheria imewekwa kwa ajili ya kumlinda mtoto chini ya umri wa miaka 18 ambaye mfumo wake wa akili unakua na haujakomaa.

"Mtoto anapojihusisha na michezo ya kamari au matumizi ya dawa za kulevya ikiwamo shisha, mfumo wake wa akili unatengeneza mazoea kwa urahisi zaidi na kuingia katika uraibu kuliko mtu mzima ambaye akili yake imekomaa anajua lipi ni sahihi na lipi si sahihi.

"Mtoto yupo kwenye kipindi cha kujaribu mambo na anapozoea anaweza kuingia katika tabia hatarishi kwa afya yake, mfano matumizi ya shisha ni hatari kwa afya na michezo ya kamari inaweza kumwingiza katika tabia za wizi ili kupata fedha za kucheza. Jamii inatakiwa kuwalinda watoto na vitu vyote ambayo ni hatarishi kwao," anasema.

Kamishna wa Kinga na Tiba kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Tanzania (DCEA), Dk. Peter Mfisi, anasema shisha ni tumbaku kama nyingine, lakini yenyewe huvutwa kwa kutumia bomba maalum.

"Shisha kama shisha ni dawa za kulevya ambazo haidhibitiwi na DCEA wanaodhibiti ni Wizara ya Afya. Lakini inapotokea mtumiaji amechanganya na dawa za kulevya kama bhangi au heroine hapo DCEA ndio tunahusika kwa sheria zetu.

"Shisha yenyewe ina kiwango kikubwa cha tumbaku ambacho mtu anapovuta pafu moja ni sawa na aliyevuta sigara 100 na husababisha uraibu," anasema.

Nipashe ilipotaka kujua mikakati ya Wizara ya Afya katika kudhibiti shisha katika makazi ya watu, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Afya, Englibert Kayombo, aliomba apewe muda afuatilie kisha angemrejea mwandishi, lakini alipotafutwa tena alisema bado anafuatilia suala hilo.

Akizungumza kama daktari, mtaalam Mfisi anasema ni vizuri serikali kutafuta uwezekano wa shisha kutouzwa kiholela.

Anashauri kutengwe maeneo maalum ya kuvuta katika hoteli na baa kubwa ambazo si rahisi mtoto kufika na wahusika wapewe leseni za muda kudhibiti na si kama sasa baadhi huduma hizo zinapatikana katika makazi ya watu.

"Uvutaji wowote wa sigara au shisha wewe unaweza ukawa unavuta unapotoa moshi nje watu wote waliokaribu na wewe wanapata athari sawa na anayevuta, Kama zinavutwa katika makazi au mtoto anavuta athari za kiafya ni kubwa zaidi," anasema.

Meneja wa Leseni na Huduma za Sheria kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Catherine Lamwai, anakanusha kwamba mashine zilizozagaa holela katika makazi ya watu ni zao.

Anafafanua kwamba Sheria ya Michezo ya Kubahatisha ya Mwaka 2003, kifungu 70 kimekataza watoto chini ya umri wa miaka 18 kucheza na kamari na kimetoa adhabu si chini ya milioni moja au kuzidi milioni tano au kifungo kisichozidi miezi 12 au adhabu zote kwa pamoja.

"Sheria inakataza mtoto kucheza kamari na hata kuonekana kwenye maeneo akizungukazunguka na pia inampa adhabu hata wewe unayemwona mtoto akizunguka ukamwacha," anafafanua.

Catherine anasema katika sheria hiyo kifungu 82 (a) kinaruhusu GBT kuteketeza mashine zinazokamatwa ambazo zipo kwenye maeneo ambayo hayako kisheria au sheria haijaruhusu kuwapo au mtu kukutwa na mashine bila leseni.

Anasema huko nyuma walikuwa na kampeni ya kuelimisha wananchi kuzitambua mashine hizo ikiwa ni pamoja na zile ambazo hazina nembo zilizotapaa katika makazi ya watu ili wazikamate.

"Zile ambazo hazijafuata utaratibu wa kisheria hazitakiwi kuwapo, zinazotakiwa ni zilizofuata utaratibu wa kisheria. Ili mtu aruhusiwe kuleta mashine hizo nchini anapaswa kuwa na leseni ya michezo ya kubahatisha kwenye mchezo husika na inapoibiwa lazima aseme," anafafanua.

Pia anasema leseni hutoka katika maeneo ambayo si karibu nyumba za kuabudu, hospitali na liwe rahisi kufikika na vyombo vya dola.

"Hazitakiwi kuwekwa katika duka la mangi (vyakula) ambako mtoto anaweza kutumwa. Lazima kuwekwe tangazo mtoto chini ya miaka 18 haruhusiwi. Tusiseme tu zimetapakaa. Je, umechukua wajibu gani kumlinda mtoto wako? umemwona mtoto wa jirani umemsaidiaje?" anahoji.

Ofisa Habari Mwandamizi GBT, Zena Athuman, anasema baada ya kubaini kuzagaa kwa mashine hizo za kamari katika makazi walianzisha Kampeni ya Mlinde Mtoto iliyofanyika 2022/23.

"Tanzania tuna kampuni 53 lakini si yote yanayoendesha hizi mashine, kampuni moja inaweza ikawa na biashara zaidi ya moja. "Wanaosajiliwa wanatakiwa kukaa kwenye baa au maduka maalum ya kuchezea na kinyume na hapo hufanyika ukaguzi kuhakikisha sehemu kama inaruhusiwa kisheria.

"Kuna watu wameibuka ambao wanaendesha hii biashara bila kufuata utaratibu, hao ndio wanaoleta shida wamezisambaza mitaani katika makazi ya watu, mashine zinazoongelewa ni zile utazikuta kwa mangi, vibarazani au kwa mama lishe," anasema.

Zena anasema mwaka 2023 walianzisha kampeni nyingine ijulikanayo kama 'Fichua Tukomeshe Mashine Haramu', inayoendelea hadi sasa kwa lengo la kuelimisha watu maeneo sahihi ya kufanya biashara hiyo kama sheria inavyoelekeza.

Anasema mashine walizosajili mpaka sasa ni 32,000 na tangu wameanza kampeni hizo watu 32 wamekutwa na hatia kisheria.

Kuhusu mapato yatokanayo na michezo ya kubahatisha, Zena anasema mwaka 2021/22 fedha iliyopatikana zilikuwa ni Sh. bilioni 144, mwaka 2022/23 Sh. bilioni 170 na 2023/24 makadirio yao ni kupata Sh. bilioni 200.

Julai 17, mwaka huu, wakati serikali ikisema imekamilisha kanzidata ya wauzaji wakubwa wa dawa za kulevya na kuanza uchunguzi.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi, alisema kila siku hospitalini hapo hupokea waraibu 900 wanaotumia dawa za usaidizi wa kuacha dawa za kulevya 'methadone'.



## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushauri wa madaktari kuhusu vyakula uzingatiwe kikamilifu

**MARA** kwa mara, madaktari wakiwamo mabigwa na wabobezi pamoja na wataalamu wa lishe, wamekuwa wakitoa ushauri kuhusu namna ya ulaji bora ili kujiepusha na maradhi hasa magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Katika kufanya hivyo, pia wamekuwa wakisisitiza vyakula bora kwa wajawazito na watoto ili kujikinga na madhara mbalimbali ikiwamo udumavu kwa watoto.

Hatua hiyo ya madaktari na wataalamu wa lishe inatokana na kasi kubwa inayoendelea sasa ya watu kupatwa na maradhi yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari, saratani, shinikizo la juu la damu na maradhi ya moyo. Maradhi hayo kwa sasa ndiyo yamekuwa tishio kubwa kwa afya za watu wengi na yamekuwa chanzo kikubwa kwa vifo vya maelfu ya watu hasa katika nchi zinazoendelea, Tanzania ikiwamo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Dk. Mohammed Janabi, kwa mfano, amekuwa akihimiza namna watu wanavyotakiwa kula huku akihimiza watu kupunguza ulaji wa baadhi ya vyakula kama vile nyama nyekundu, vyakula vya wanga mafuta na sukari pamoja na unywaji wa pombe huku akisisitiza kwamba ni hatari kwa afya. Pamoja na msisitizo huo, baadhi ya watu wamekuwa wakibeza na hata kukejeli kuwa wanapokula vyakula hivyo na kunywa pombe, wanachangia pato la taifa.

Kama wahenga wasemavyo mzaha mzaha hutumbuka usaha, ndivyo inavyokuwa kwa sababu kuendelea kupuuza ushauri huo wa madaktari, ndivyo hatari inavyozidi kwa kuwa idadi ya watu wanaougua magonjwa hayo inaongezeka. Sababu kubwa ni kupuuza ushauri huo hata ule wa watu kutakiwa kufanya mazoezi.

Wakati hayo yakiendelea kwa wataalamu kuhimiza ulaji bora wa vyakula na kuepuka baadhi ya vyakula ili kupambana na maradhi, limeibuka tishio lingine kuhusu mfumo wa ulaji vyakula. Kwa mujibu wa Bingwa wa Upasuaji na Mkuu wa Idara ya Upasuaji Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Mloganzila, Dk. Eric Muhumba, watu wanaokaa muda mrefu bila kula, wako hatarini kupata vidonda vya tumbo (ulcers).

Kadhalika, anasema watu wanaokula mlo kupitiliza bila kuzingatia lishe, wamo hatarini kuingia kwenye kundi la walio na unene uliopindukia (obesity). Kwa mujibu wa Dk. Muhumba, Unene uliopindukia kitaalamu hutokea wakati fahirisi ya uzito wa mwili (body mass index) wa mtu ni 30 au zaidi.

Mtaalamu huyo anasema kundi la watu wanaoshinda njaa muda mrefu, wamo hatarini kupata vidonda vya tumbo, kutokana na aside (tindikali) iliyomo tumboni na kwamba sababu kuu ya vidonda vya tumbo ni asidi nyingi tumboni ambayo inazalishwa unaizalisha wewe mwenyewe. Sababu ya kuwa na vidonda ni maambukizi ya bakteria wanaoitwa Helicobacter pylori (H. Pylori).


Aidha, kwa mujibu wa mtaalamu huyo, hatari ya aside inayozalishwa kwa wingi tumboni hutokana na mtu kutokula muda mrefu, kula vyakula vinavyozalisha kemikali hiyo pamoja na msongo wa mawazo, huweza kusababisha utumbo kutoboka na kuhitajika upasuaji wa dharura. Pia anasema mtu kukaa na njaa muda mrefu, kunasababisha acid inakuwa yenyewe tumboni inaanza kula kuta za tumbo.

Taarifa hii ya mtaalamu huyo bingwa wa afya, inapaswa kuzingatiwa kwa watu kufuata utaratribu bora wa ulaji wa vyakula badala ya kupuuza na kuona ni jambo la mzaha. Wako watu ambao muda mwingi wamekuwa hawali vyakula, pengine siku nzima huku wakisema wanaweka miili yao sawa bila kujua wanahatarisha afya zao pamoja na kufupisha maisha yao.

Wataalamu wa maandiko matakatifu wanasema Mwenyezi Mungu hutumia watu tofauti kuwakumbusha wanadamu kuishi maisha mema, hivyo ni dhahiri kwamba kauli za madaktari kuhusu masuala ya afya ni mwendelezo huo na watu wanatakiwa kuyafuata ili kujiepusha na maradhi yanayoweza kukatisha uhai wao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wamachinga watatuliwe kero waende katika masoko

**SERIKALI** imejitahidi kujenga masoko kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo, maarufu kama wamachinga, katika mikoa mbalimbali nchini ili kuwa na sehemu na kufanya biashara zao bila bughudha.

Miongoni mwa mikoa ambayo serikali imejenga masoko hayo ni Dar es Salaam, yakiwamo ya Makumbusho, Simu 2000, Mbezi, Kinyerezi na Mbagala.

Pamoja na jitihada hizo, mengi kati ya hayo, yako tupu bila wamachinga huku wengi wao wakifanya biashara kandokando ya barabara au maeneo mengine ambayo ni hatarishi kwao.

Katika mazingira hayo, ni wazi kwamba serikali itakuwa inaingia hasara kutokana na ujenzi wa masoko hayo ambayo yanakuwa na wafanyabiashara wachache huku wengine wakiwa barabarani.

Mfano, niliwahi kwenda katika soko la Mbezi Mwisho karibu na kituo kikuu cha mabasi ya mikoani cha Magufuli ambalo viongozi wake walisema lina uwezo wa kuchukua wafanyabiashara 800.

Viongozi wakasema pamoja na uwezo huo, lina wafanyabiashara 50 tu na kwamba wengine 750 waendelea na biashara maeneo mengine ya Mbezi yakiwamo ya kando ya barabara.

Ninadhani kwa hali kama hii, kuna haja ya serikali na wafanyabiashara kukaa meza moja kujadili kwa kina ili kujua kwa nini wamekuwa wagumu kwenda kwenye masoko hayo.

Kupitia njia hiyo ya kukaa pamoja ili waeleze sababu za msingi za kushindwa kwenda katika masoko yao, kunaweza kusaidia kuleta suluhu kwenye jambo hilo ambalo limeonekana kushindikana.

Baadhi yao hudai kuwa hawaendi katika masoko hayo, kutokana na kwamba hawakushirikishwa wakati wa ujenzi au kabla ya ujenzi na kwamba ujenzi umefanyika katika maeneo ambayo si rafiki kwao.

Kwa hali kama hiyo, ninadhani njia ya kutatua changamoto za wamachinga hao ni viongozi wao kukutana na serikali ili kuweka mambo sawa ili kila upande uwezo kutimiza wajibu wake.

Iwapo watahamia katika masoko hayo, itakuwa ni rahisi kwa serikali kukusanya ushuru, lakini pia watakuwa salama zaidi kuliko ilivyo sasa, ambapo wengine wanapanga bidhaa katika mazingira ya hatari.

Fikiria mtu anapanga biashara chini ya nyaya za umeme mkubwa au kando ya barabara. Mazingira kama hayo si rafiki ni hatari kwa usalama wao ingawa wenyewe ni kama hawajali.

Wamachinga wana umuhimu wao katika kukuza uchumi wa nchi, lakini wakiachwa wanazagaa tu inaweza ikawa ni vigumu kwa serikali kupata kodi kutoka kwa wafanyabiashara hao.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wamachinga ni watu muhimu katika kukuza pato la taifa, na kwamba takwimu zinaonyesha kuwa sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo vimetengeneza ajira, kukuza uchumi na kuondoa umaskini.

Amewahi kukaririwa na vyombo vya habari akisema, sekta hiyo ina jumla ya wajasiriamali milioni 3.1, walioajiriwa ni asilimia 23.4 ya nguvu kazi ya taifa na imechangia asilimia 27 katika pato la taifa.

Ninadhani kwa umuhimu wao huo kwa taifa, ipo haja kwa pande hizo mbili kukaa pamoja ili kufanikisha mipango ya kuwaondoa maeneo hatari, lakini pia serikali iweze kufaidika na kuwapo kwao.

Sio siri kwamba wamachinga ni fursa sahihi ya kujenga uchumi, lakini pia ni vyema mazingira yao ya kufanyia biashara yakaboreshwa, ili wasiwe na kisingizio cha kutokwenda katika masoko mapya.

Njia hiyo ya kukaa pamoja huku wamachinga wakielezea vikwazo vyao, utekelezaji wake utakuwa ni muarobaini wa yale yanayowakabili wafanyabiashara hao wadogo waliotapakaa nchi nzima.

Inasikitisha kuona serikali ikituma gharama kubwa kujenga masoko kwa ajili ya wafanyabiashara hao, halafu wenyewe hawayatumii kana kwamba hakuna gharama yoyote iliyotumika kujenga.

MAKALA

FIKRA MBADALA

# Wasaidizi wanamweleza ukweli Rais Samia?



Pascal Mayalla

KAMA kawa, kila nipatapo fursa, huja na makala elimishi kwa maslahi ya taifa ambazo huwa na maswali, hoja, majibu. Swali la leo ni kuhusu wasaidizi wa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano. Dk. John Magufuli (JPM). Wateule hawa, kama inavyojulikana kwamba Urais ni taasisi na si mtu, walipewa dhamana ya kumshauri katika masuala mbalimbali.

Badala ya kufanya hivyo, walikuwa wanamwogopa hadi kushindwa kumsaidia,na matokeo yake akafanya mambo kadhaa yaliyokwenda kinyume cha Katiba, ikiwamo kupiga marufuku mikutano ya siasa, hadi alipoingia Rais Samia Suluhu Hassan, akarekebisha.

Swali linakuja kwa Rais Samia. Je, wasaidizi wake nao pia wanamwogopa hadi kushindwa kumsaidia au wanafanya kazi yao ipasavyo? Inawezekana na ni wazi kwamba Rais Ramia ana nia ya dhati kuona Tanzania inakuwa ya mani na utulivu na watu wake wanaishi wa upendo na mshikamano lakini wasaidizi wake wakashindwa kumsaidia katika baadhi ya mambo.

Suala la Katiba, kwa mfano, Rais Samia anajua kuwa ina ubatili fulani uliochomekewa kiubatili, hivyo kuifanya Tanzania kuwa na Katiba batili? Je, anajua kuwa sheria mpya ya uchaguzi aliyotia saini hivi karibuni ni sheria batili inayokwenda kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977? Je, anajua ubatili huu unadhulumu haki ya Mtanzania kuchagua na kuchaguliwa?

Hili sharti la wanasiasa kudhaminiwa na chama cha siasa ili kugombea uongozi ni batili na liko kinyume cha Katiba ya JMT ya mwaka 1977 na limechomekewa kiubatili ndani ya Katiba yetu.

Ubatili huu unamaanisha Katiba yetu ina ubatili na sheria mpya ya uchaguzi ni batili. Serikali imetunga muswada batili, Bunge letu likatunga sheria batili, na Rais akaisaini hiyo Sheria batili kuanza kutumika, kwanini serikali yetu itunge muswada wa sheria batili?, kwanini Bunge letu tukufu litunge sheria batili? Kwa nini Rais wetu asainishwe sheria batili wakati wasaidizi wa Rais sheria wapo?

Japo Rais wa Tanzania ana kinga ya kikatiba ya kutokushitakiwa kwa makosa yoyote atakayotenda akiwa madarakani katika utekelezaji wa majukumu yake, Ibara ya 56A imesema kinagaubaga kuwa kinga hiyo ya Rais kutokushitakiwa, inahusu makosa mengine yote ila haihusu anapovunja Katiba ya JMT, hivyo anashitakiwa kwa mujibu wa ibara ya 56A.

jambo ambalo tunaweza kumsamehe Rais kwa kutia saini sheria batili kuanza kutumika, ni kwa vile si mwanasheria, hivyo hategemewi kuujua ubatili wa Katiba. Lakini kwa vile ana wasaidizi wake wa sheria, wakiongozwa na Waziri wa Sheria na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambao ni manguli wa sheria, wabobezi na wabobevu ambao wanaujua kabisa ubatili wa sheria hiyo, hawajamweleza Rais kuhusu ubatili huuuliofanywa na awamu zilizotangulia. Rais Samia kaingia kaukuta, hivyo wakamtungia tu sheria batili kwa sababu sheria ikiyokuwapo nayo ni batili lakini ilikuwa inatumika!

Kuna kanuni ya 'the doctrine of separation of powers' kati ya mihimili inayokwenda na kitu kinachoitwa 'checks and balance' inayoitaka kila mhimili kuwa kiranja wa mhimili mwenzake kuwa usikiuke mamlaka yake wala usikiuke katiba.

Ibara ya 64 (5) ya Katiba imetamka wazi kuwa Katiba ndiyo sheria mama. Sheria nyingine yoyote itakayokinzana na katiba, itakuwa batili. Anayebatilisha sheria batili si Mahakama bali ni katiba yenyewe. Jukumu la Mahakama ni kuthibisha tu huo ubatili na kutangaza kuwa ni batili. Tangu siku Mahakama Kuu ya Tanzania ilipouthibitisha ubatili huu na kuutangaza, kuanzia hapo ubatili huo unakuwa umeishabatilika hapo hapo kuanzia saa hiyo.

Licha ya Mahakama Kuu ya Tanzania kuutangaza ubatili huu na kuubatilisha, serikali ya awamu ya sita, bado imetunga muswada wa sheria wenye ubatili ule ule na Bunge letu likaupokea muswada huo batili na kuutungia sheria hali iliyowafanya wabunge wetu makini kugeuka kama si makini. 'Checks and balance' inatoka wapi?

Bunge letu chini mwalimu wangu wa sheria pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), mwanasheria mbobezi na mbobevu, Dk. Tulia Akson, lilipaswa kuieleza serikali kuwa haiwezi kututungia muswada batili na Bunge lina mamlaka ya kuuondoa ubatili huo na kutunga sheria safi isiyo na ubatili. Pamoja na ukweli huo, Bunge letu likatunga Sheria batili na kumpelekea Rais Samia kuitia saini. Je, Rais Samia anajua kuwa amesainishwa sheria batili?

Kwa vile Rais Samia anawaamini sana wasaidizi wake, wamemtungia muswada batili na Bunge likitunga sheria batili, Rais Samia akaamini kuwa anatia saini sheria halali bila wasaidizi wake kumweleza ukweli kuwa sheria hiyo ni batili. Kwa hiyo kwenye hili la ubatili wa sheria mpya ya uchaguzi, Rais Samia hana kosa kabisa bali ni serikali kutunga muswada batili na bunge kutunga sheria batili.

Swali la kujiuliza ni baada ya kelele zote hizi kuhusu ubatili wa Katiba yetu na ubatili wa sheria zetu, je, Rais Samia amezisikia? Nasema hivyo kwa sababu

naona maandalizi ya uchaguzi wa serikali za mitaa kwa sheria batili yanaendelea na mwakani tunakwenda kwenye uchaguzi mkuu na katiba batili na sheria batili.

Naamini kabisa kuna siku iso jina, kilio hiki cha haki kitasikika. Mungu Mbariki Rais Samia, jicho lake liione hii dhulma kubwa ya haki ya Mtanzania kuchagua na kuchaguliwa airejeshe.

**Mungu Ibariki Tanzania**
**Paskali +255 754 270403**

# Daktari aingia matatani madai ya kumwomba rushwa mjamzito

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

MGANGA wa Kituo cha Afya Ndago kilichoko wilayani Iramba mkoani Singida, Dk. Japhet Nkwabi, ameingia matatani baada ya Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, kuiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kumchukulia hatua kwa madai ya kuomba rushwa ya Sh.152,000 kwa mjamzito.

Aidha, mkuu huyo wa wilaya amemwagiza Ofisa Utumishi na Rasilimali Watu Halmashuri ya Wilaya Iramba kumchukulia hatua za kinidhamu kwa makosa ya kutomtii mkuu wake wa kazi na kutokuwapo kwenye kituo chake cha kazi kwa zaidi ya wiki tatu.

Mwenda alitoa agizo juzi katika kikao kazi cha watumishi wa halmashauri hiyo ambacho kilikuwa na lengo la kufanya tathmini ya mafanikio na changamoto ya kila idara kwa mwaka wa fedha uliopita 2023/24.

"Haiwezekani serikali inatoa huduma za wajawazito bure lakini huyu mtumishi amekuwa akiwaomba kinamama rushwa ili kuwahudumia. Hivi karibuni alikuja mama mjamzito kutoka kijiji cha Mtekente alitaka kupata huduma ya kujifungua lakini daktari huyu alimwambia bila kumpa Sh. 152,000 hawezi kumzalisha," alisema.

Mwenda alisema huduma za afya kwa mjamzito kwa mujibu miongozo ya Wizara ya Afya, zinatolewa bila malipo yoyote na mtumishi yeyote wa afya atakayemwomba rushwa mjamzito, atachukuliwa hatua.

"Nimekuwa nikipokea tuhuma nyingi dhidi ya daktari huyu kwa watu mbalimbali pia amekuwa hamheshimu mkuu wake wa kazi mganga mfawidhi wa kituo chake, Dk. Ahmad Selemani, kwa kigezo wana elimu sawa," alisema.

Alisema daktari huyo katika kuonyesha hamtii mkuu wake wa kazi, ameondoka kituoni kwake kwenda Dar es Salaam bila ruhusa kutoka kwa mkuu wake kituoni wala ruhusa kutoka kwa mwajiri wake.

Aidha, Mwenda alielezea kuchukizwa na kitendo cha uongozi wa Hospitali ya Wilaya ya Iramba kumhamishia daktari huyo Hospitali ya Wilaya kutoka Kituo cha Afya Ndago.

"Kama daktari anaomba rushwa kwa wagonjwa na kuwaambia bila kutoa pesa hawezi kuwahudumia na mnaamua kumleta Hospitali ya Wilaya huku si ndiyo atawamaliza wagonjwa wengi" alihoji.

# Waziri akerwa uharibifu vyanzo vya maji

**Na Lusungu Helela,** KIBAKWE

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora , George Simbachawene, amekerwa na wananchi wanaoendesha shughuli za kilimo katika milima ya Kibakwe.

Kutokana na kuwapo kwa vitendo ghivyo, Simbachawene ambaye pia ni Mbunge wa Kibakwe, amesema ana hofu kama hatua za haraka hazitachukuliwa vyanzo vya maji vitakuwa hatarini kutoweka.

Simbachawene alisema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi kwa nyakati tofauti kwenye mikutano ya hadhara iliyofanyika katika vijiji vya Lutarawe, Njiapanda na Kikuyu, Kibakwe wilayani Mpwapwa huku akibainisha kuwa vyanzo hivyo vya maji ni tegemeo pekee kwa wakazi wa jimbo hilo.

Alisema maji yanayotoka katika milima hiyo yana manufaa makubwa kwa watu wote ilhali mazao yanayolimwa katika milima hiyo ni kwa ajili ya manufaa ya watu wachache.

Simbachawene alisema pamoja na vyanzo hivyo kuwa tegemeo, kasi ya ukataji miti inazidi kushamiri juu ya milima hiyo kwa ajili ya kilimo, hali inayotishia maisha ya watu wote kwa sababu ya maslahi ya watu wachache.

Kutokana na hali hiyo, Simbachawene aliwataka madiwani kwa kushirikiana na viongozi wa vijiji, kuzungumza na wanaolima juu ya milima hiyo na kama hawatawaelewa basi sheria kali zichukuliwe dhidi yao kwa kuwa wanahatarisha uhai wa wananchi wa Kibakwe na taifa kwa ujumla.

"Milima mingi imebaki vipara, miti mingi imekatwa kwa ajili ya kilimo hali inayochangia wakati wa mvua maji kushuka kwa kasi kutoka milimani na kusababisha uharibifu wa miundombinu ya Barabara.

Hii si sawa kabisa, nawaagiza viongozi chukueni hatua za haraka kwani mnawajua kwa majina wanaoyafanya hayo," alisisitiza.

Kutokana na uharibifu huo, Simbachawene alisema tatizo la maji katika jimbo hilo halitaisha hata kama serikali itatoa fedha kwa vile vyanzo vya maji vinazidi kuharibiwa.

Simbachawene alisema juhudi zinazofanywa za kuwapelekea miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya, shule, barabara na umeme haitakuwa na maana kama vyanzo hivyo vitatoweka kwa kuwa maji ni uhai.

# Simbachawene aahidi mageuzi katika kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** KIBAKWE

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, ameahidi kuwaletea wananchi wa Kibakwe mradi wa kimkakati wa umwagiliaji.

Sambamba na mkakati huo, Simbachawene ambaye ni Mbunge wa Kibakwe, amewataka wananchi wa jimbo hilo kuendesha kilimo cha kibiashara kwa kutumia miundombinu ya umeme iliyopo. Simbachawene alisema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi kwa nyakati tofauti kwenye mikutano wa hadhara iliyofanyika katika vijiji vya Idodoma na Malolo, ikiwa ni mwendelezo ziara yake ya kikazi katika jimbo hilo.

Alisema hatua ya umeme kufika katika vijiji hivyo itachochea mapinduzi makubwa, hivyo ni muda mwafaka kuhakikisha unatumika kuendesha mashine ya kusukuma maji ya kumwagilia mashambani.

Alisema awali changamoto kubwa ilikuwa kilimo cha umwagiliaji cha kutumia dizeli na petroli ambayo ilikuwa ngumu kuona tija kutokana na gharama kubwa ya nishati hiyo. Aliongeza kuwa umwagiliaji umekuwa duni kutokana na mifereji inayotumika kuwa ni ya kizamani na inachangia upotevu mkubwa wa maji.

"Tunataka mabadiliko makubwa katika jimbo letu, tunatamani kuona umeme tulionao unatupeleka mashambani na sio kuutumia tu kwa ajili ya kuwashia taa pekee majumbani mwetu," alisema.

Alisema umeme huo utumike kusukuma maji ya kumwagilia usiku na mchana katika mashamba ya wananchi huku akisema miaka 10 ijayo anaviona vijiji hivyo vikiwa katika viwango vya juu kiuchumi.

Naye mkulima Aidani Chihoma alitumia fursa hiyo kumshukuru Waziri Simbachawene kwa kupeleka umeme katika vijiji hivyo huku akisema ujio huo wa mradi huo wa umwagiliaji utasaidia kuona tija ya kilimo cha vitunguu na maharagwe.

Vijiji vya Idodoma na Malolo ni miongoni mwa vijiji katika Jimbo la Kibakwe vinavyosifika kwa kustawisha zaidi kilimo cha vitunguu na maharagwe ambapo uhitaji wa mazao hayo umekuwa mkubwa ndani na nje ya nchi.

# Wananchi wasimulia adha ukosefu mtandao

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

WAKAZI wa kijiji cha Ngokolo, Kata ya Bukomela Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama, walioishi miaka yote bila kuwa na huduma ya mawasiliano, wameeleza hali hiyo ilivyowatesa hadi kuwalazimu kuitafuta kwa kupanda juu ya miti na milimani.

Walieleza hayo juzi kwa nyakati tofauti wakati wa uzinduzi wa mnara wa mawasiliano katika maeneo hayo uliozinduliwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, huku wakisema hatua hiyo imewasaidia kuondokana na adha hiyo.

Mmoja wa wananchi hao, Joseph Mabala, alisema kijijini hapo hapakuwa na mawasiliano kabisa na kwamba walikuwa wakipanda juu ya miti na milimani ndipo wapate kuwasiliana.

"Tunashukuru kupata mnara wa mawasiliano hapa kijijini, tatizo la kupanda juu ya miti na milimani halipo tena, sasa hivi tunawasiliana tu sehemu yoyote," alisema Mabala.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema hali ya mawasiliano jimboni humo si nzuri kutokana na ukosefu wa minara na kuwa waliomba kuwekewa minara saba lakini iliyokamilika ni minne na kusalia mitatu na kumwomba waziri kukamilishwa kwa iliyosalia. Waziri Nnauye alisema kwa sasa wanatekeleza mradi wa nchi nzima ujulikanao kama Tanzania ya kidijitali kwa kujenga minara 758 katika mikoa 26 Tanzania Bara, ili kurahisiha hali ya upatikanaji wa mawasiliano hasa maeneo ya vijijini ambayo hayakuwa na huduma hiyo matarajio yakiwa kuwafikia Watanzania milioni 8.5.

Alisema katika mkoa wa Shinyanga, inajengwa minara 30 na katika jimbo hilo itajengwa minara saba na kwamba minara minne tayari imekamilika na kusalia mitatu ambayo nayo itakamilishwa kujengwa hivi karibuni na kuwashwa.

Aidha, aliwatahadharisha wananchi wa kijiji cha Ngokolo na maeneo mengine ambayo minara hiyo tayari imeshawashwa na kupata mawasiliano, kwamba wachukue tahadhari kuepukana na matapeli wa mitandaoni wakiwamo wa tuma kwa namba hii ili kutotapeliwa pesa zao wakiwamo na wastaafu.

Pia aliwasihi vijana wasitumie mitandao ya kijamii kwa matumizi yasiyo sahihi, kwa kuchafuana na hata kutukana viongozi, ili wasije ingia kwenye mikono ya sheria.



Mkurugenzi wa Milki wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Upendo Matotola (katikati), Mkurugenzi wa Kampuni ya TT Investments, Yongjun Liu (kulia), na Mwakilishi wa kampuni ya REMAX Coastal Reality, Happiness Watimanywa, wakibofya kitufe wakati wa uzinduzi rasmi wa mradi wa nyumba za kisasa wa, Phoenix Condo, eneo la Masaki Jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mndeme ataka makazi nishati safi mpango jinsia mabadiliko tabianchi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, anayeshughulikia Mazingira, Christina Mndeme, amewasisitiza wadau wa mazingira kuweka mkazo suala la nishati safi ya kupikia katika Rasimu ya Mpango Kazi wa Taifa wa Masuala ya Jinsia na Mabadiliko ya Tabianchi.

Amesema wanawake nchini hutumia muda mwingi kutafuta kuni kwa ajili ya kupikia badala ya kufanya shughuli za kujiingizia kipato. Kutokana na hali hiyo, alisema ni muhimu kupanga mipango ya kushirikisha nishati safi katika masuala ya kijinsia.

Mndeme alisema hayo juzi wakati akifungua Kikao kazi cha Wadau cha Kukusanya Maoni Kuhusu Rasimu ya Mpango Kazi wa Taifa wa Masuala ya Jinsia na Mabadiliko ya Tabianchi, jijini Dodoma.

Alisema athari za mabadiliko ya tabianchi yameathiri sekta za kiuchumi ambazo wanawake, wanaume, watoto, wazee, vijana na makundi maalum hutegemea kwa maisha yao ya kila siku.

Mndeme alisema sababu mbalimbali, zikiwamo majukumu yao kijinsia, utamaduni, umri, uchumi, mila na desturi huchangia makundi hayo ya jamii kuathirika na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Hii ni hatua kubwa katika uwezeshaji wa masuala ya jinsia hapa nchini, kama mnavyofahamu.

Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi, Itifaki ya Kyoto na Makubaliano ya Paris. Makubaliano ya Paris yanazitaka nchi wanachama kuandaa Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Programu ya Lima kuhusu masuala ya Jinsia na Mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Mkataba huo ulianzishwa mwaka 2014 katika mkutano wa 20 wa Nchi Wanachama wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP20) uliofanyika Lima, Peru. Madhumuni ya LWPG ni kuzihimiza nchi Wanachama wa Mkataba kuhuisha masuala ya jinsia katika mipango kazi ya kitaifa ili kutekeleza Mkataba na Makubaliano ya Paris.

Katika utekelezaji wa mkataba huo,Ofisi ya Makamu wa Rais ni kiungo wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi nchini, inaratibu maandalizi ya Mpango Kazi husika.

Mndeme alisema utafiti mbalimbali umeonyesha nchi zinazoendelea bado hazijahuisha Programu ya Lima katika mipango, sera na mikakati ili kuwezesha kuwa na takwimu za makundi hayo, usawa wa kijinsia, uwezeshaji wanawake katika majadiliano ya kimataifa, uhuishaji wa masuala ya jinsia katika sera, mipango na mikakati ya Taifa na kujenga uwezo wa kifedha, utaalam, fedha na taasisi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Serikali tayari imehuisha masuala ya Jinsia na Mabadiliko ya Tabianchi katika Sera ya Taifa ya Mazingira (2021), Mpango Kabambe wa Mazingira (2022-2032), Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (2021-2026) na Mchango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (2021-2026).

Maandalizi ya Mpango Kazi wa Taifa wa Masuala ya Jinsia na Mabadiliko ya Tabianchi ni mwendelezo ya jitihada za serikali katika kukabiliana na mabadiliko ya tabainchi kwa kwa makundi yote ya kijamii ili kuleta maendeleo endelevu nchini.

# MAISHA

JULAI 21, 2024
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 13

FULANA NYEMBAMBA
**Vazi la mahaba zaidi**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**
Weka mfumo imara kuepusha majanga ya moto



Ukurasa 12

**HARUSI**



# Alovera hung'arisha ngozi

Ukurasa 14

# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 24 | 25 | 26 | 10 | 11 | 12 |
| 71 | 72 | 73 | 51 | 52 | 53 |
| 42 | 43 | 44 | 31 | 32 | 33 |
| 15 | 16 | 17 | 19 | 20 | 21 |
| 89 | 90 | 91 | 66 | 67 | 68 |
| 57 | 58 | 59 | 87 | 88 | 89 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S | | S | I | A | S | A |
| H | | | | K | | C |
| A | | I | L | I | | H |
| N | T | A | | L | O | A |
| G | | M | E | I | | N |
| W | | K | | | | G |
| E | L | E | Z | A | | E |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

BEE, NOA, GOA, YAI, PEMBA, ATOKE, BANDO, MBEYA, SINGIDA, ATWISHE

## TOA TOFAUTI 5





## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI

KATI YA HERUFI A, B NA C NI IPI INAWEZA KUIFIKIA HERUFI Z?
TAFUTA NJIA




Alichokifanya daktari

MTOTO John alikwenda sokoni kununua samaki ambaye alitumwa na mama yake.

Alipofika alimkuta mchuuzi akiuza samaki aina ya kambale juu ya meza yake ya mbao.

**John:** Nataka samaki mkavu anauzwa bei gani?

**Mchuuzi:** Shilingi 1000 na 5000

**John:** Mi nataka aliyenyooka na sio huyu aliyejikunja

**Mchuuzi:** Hawa wamekunjwa baada ya kuvuliwa, hakuna wengine.

**John:** Kama hivyo punguza bei kwani urefu wake umepungua

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mwanamume jitie nguvu kuepuka kufa mapema

***KARIBU tena msomaji wangu kwenye mada zetu hizi nzuri za Maisha Ndivyo Yalivyo. Bado tunaelea kwenye maeneo yanayotesa ndoa nyingi katika jamii yetu. Wengi wanagugumia maumivu wasijue cha kufanya na hawatafuti chanzo chake.***

Wiki iliyopita, nilitoa simulizi ya baba mmoja mstaafu ambaye ndoa yake imetikisika mara tu baada ya yeye na mkewe kustaafu. Akasema walistaafu wote mwaka 2019 na wote walikuwa walimu.

Baba huyu tulikutana benki tumekaa kila mmoja akisubiri huduma. Cha ajabu, akasema vile ambavyo alitarajia kuwa baada ya kustaafu maisha kuendelea kuwa mazuri kwa mafao yao wote kuwa msingi mzuri, ikawa tofauti.

Huko nyuma kila mmoja alikuwa akionyesha mshahara wake na kupangilia matumizi yake. Lakini baada ya kustaafu na mafao kutoka, mkewe akawa kimya na wala hakutaka mume ajue chochote kuhusu mafao yake. Akimuuliza anakuwa mkali jambo ambalo lilimshangaza.

Akaniuliza, ni kwa nini wanaume wanakufa mapema na kuwaacha wanawake? Swali hili nilijaribu kumjibu na ushauri ndiyo umebebwa kwenye makala hii. Kwanza nilimwambia hayo mawazo aliyo nayo kuhusu mkewe kuvunja makubaliano ya pamoja kuhusu matumizi ya mapato yao ni moja ya chanzo.

> **Na katika kudadisi aligundua kuwa mkewe alipata mafao takriban milioni 120/=, lakini hivi karibuni aligundua nyaraka inaonyesha salio la mkewe benki ni milioni 35/= tu.**

Kwa maelezo yake, baba huyo alikuwa anampenda sana mkewe, hivyo kumbadilikia uzeeni ni jambo la kumshangaza sana. Baba ana umri wa miaka 75 na mkewe ni miaka 69.

Fikiria tangu mwaka 2019 walipostaafu hadi sasa, mama hajamwambia mumewe alipata mafao kiasi gani na hadi sasa amefanyia nini. Baba huyu anasema mkewe kule mwanzoni baada ya kustaafu alifanyia nyumba yao ukarabati mdogo na kununua baadhi ya vitu.

Na katika kudadisi aligundua kuwa mkewe alipata mafao takriban milioni 120/=, lakini hivi karibuni aligundua nyaraka inaonyesha salio la mkewe benki ni milioni 35/= tu. Anajiuliza fedha zingine amepeleka wapi? Na sasa ni mkali yuko kama amechanganyikiwa.

Baba huyu akasema: "Nimeamua kumwacha huko mkoani na wajukuu zetu, mimi nafuatilia miradi yangu, naandika vitabu vya shule, nina nyumba zangu kadhaa baadhi nimeuza, nyingine nimepangisha."

Ndipo nikamtia moyo nikamwambia ajitie nguvu kama mwanaume na kiongozi wa familia. Nikamshauri avae ujasiri na kufanya yale aliyokusudia katika umri alio nao sasa.

Alinde kile alichokiamini na kukisimamia bila hofu. Awe na tumaini kuwa haijalishi ni mazingira gani anapitia kwani ni lazima atimize kusudi, na kwamba asiogope japo ni nyakati nguvu.

Msomaji wangu, kwa nini namwambia baba huyu na wengine kujitia nguvu? Baba yetu wa mbinguni anakupenda sana na anakuthamini. Alikuumba kwa namna ya ajabu na kuwekeza vitu vingi vizuri ndani yako.

Kama vile alivyomwumba Adamu na kusema ni "kitu chema", ndivyo anavyokuona wewe. Mungu ana kuthamini ameweka vitu vingi ndani yako. Na kama mtoto hupaswi kumvunja moyo maana anakutegemea!

Kuna mambo mengine utapaswa kuyafanya wewe wala si mtu mwingine. Kuna wakati hupaswi kuwa tegemezi kwa watu wengine bali usimame wewe kama wewe kufanya jambo fulani.

Kama baba, usiruhusu vitu hivi; kuvunjika moyo, majuto, kukandamizwa na hofu kwani ni wezi wa hatma. Vitu hivi vimeiba furaha ya wengi, vimechelewesha hatma na kuangamiza maisha ya wengi. Hivi vikikushambulia vitahakikisha vinanyonya nguvu zako zote za kiroho na kimwili na ili usiwe mwathirika lazima ujitie moyo.

Unapojitia moyo utapata nguvu na kuvishinda na kusonga mbele kwenye hatma yako. Baba ninayemjadili katika maelezo yake nimeona akijitia nguvu. Baada ya kujua yaliyojificha kwa mkewe, amepata nguvu mpya kuwa bize na miradi yake hapa Dar na huitembelea familia yake hiyo huko mkoani na kurejea.

Hapa alichoamua ni kujitia nguvu mwenyewe ili asipoteze fursa kwenye maisha yake ya kustaafu. Ni kwa sababu upo wakati lazima ujitie nguvu ya kuendelea ili usipoteze ndoa yako na pia biashara ya ndoto yako.

Isitoshe, wakati kuna matatizo kwenye ndoa yake, utapaswa kujitia nguvu ya kuendelea na kusimama ili watoto wako na wajukuu wasiathirike na matatizo yenu.

Hapa nimegusia eneo moja tu, kujitia nguvu kuepuka kifo cha mapema kwa wanaume. Mengine ni uchawi, mizimu, misingi mibovu ya familia. Haya tujadili wiki ijayo.

***Je, una maoni, Kisa? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi

# Wimbi hili wenye ulemavu 'ombaomba' tishio kiuchumi

KUNA msemo kwamba katika maisha usipopambana, kuomba kunadhalilisha. Kibaya zaidi kuomba inakuwa aibu ya kwanza. Kunyimwa unachotaka inakuwa aibu ya pili na kutangazwa inakuwa aibu ya tatu.

Hii inatufundisha nini? Pambana sana kutafuta fedha maana umasikini unadhalilisha mno.

Ulemavu hujumuisha walio na changamoto za kimwili, kiakili na kihisia za muda mrefu ambazo zinapoingiliana na vikwazo vya kimitazamo, kimazingira na kitaasisi, hufanya iwe vigumu kwa mtu kushiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika shughuli za jamii sawa sawa na wengine.

Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010 kwa Tanzania Bara na Sheria ya Watu wenye Ulemavu (Haki na Fursa) ya Mwaka 2006 kwa Zanzibar, zote zinawatambua wenye ulemavu na kuwaweka kwenye mipango ya huduma mbalimbali, haijalishi mahali wanapoishi au jinsi zao.

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuhusu uwezeshaji kwa jamii ya watu wenye ulemavu, inaonyesha kuwa kwa mwaka 2022/23 na 20/24, watu wenye ulemavu waliotambuliwa walikuwa 154,844.

Kati yao wanawake ni 76,178 na wanaume ni 78,666 ambao walitambuliwa na kufanyiwa tathmini. Licha ya kutambuliwa na kufanyiwa tathmini, pia walipewa huduma za mahitaji mbalimbali.

Licha ya kuwapo jitihada mbalimbali za kuwainua kiuchumi, watu wenye ulemavu wanapata ukosefu wa ajira mara mbili ya kiwango cha wale wasio na ulemavu.

Sijui unanielewa? ni hivi! Hisani imepuuza njia ambazo sera na mifumo iliyopo inawatenga na au kuwaadhibu wenye ulemavu na kuwanyima usalama wa kiuchumi.

Ni wazi kwamba ufadhili hauwezi kuendeleza haki ya kiuchumi bila ya kujumuisha lenzi ya ulemavu.

Tuwape nafasi katika miradi ya kiuchumi, na serikali ijikite zaidi kuhusianisha sera na mipango na uwezeshaji kiuchumi ili kuwaondoa jamii hii katika utegemezi wa kipato.

Huko mitaani, mijini na hasa katikati ya mji na vituo vya mabasi, kuna idadi kubwa ya watoto, vijana na wazee wanaozunguka kutwa nzima wakiomba pesa.

Hakuna anayewaona na kutafuta ufumbuzi wa kuwaondoa mitaani, ili kuacha kuombaomba pesa kila uchao.

Mbona Halmashauri zetu zikijipanga wanaweza kujenga mwitikio wa pamoja wa kuwajumuisha kupata miradi katika sekta mbalimbali.

Pasina shaka, watu wenye ulemavu wanapata changamoto kupata maeneo ya kufanyia shughuli za uzalishaji mali, kama kwenye masoko ya walaji lakini haizuii wao kupambana kutafuta na kuvuja jasho ili kukuza uchumi wao.

Wenye ulemavu wanaweza kujinasua huko kwa kujipa maono kwamba kuanzia sasa hatutaki kuwa ombaomba, tunataka kazi.

Kwa kuwa ugumu wa maisha, ndio kipimo cha akili, basi kazi itamwezesha kujitegemea na kupata heshima katika jamii.

Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010, Ibara ya 33, Ibara ndogo ya tatu, inasema kila mwajiri anayeweza kuajiri watu 20 ni lazima asilimia tatu, wawe watu wenye ulemavu na atengeneze miundombinu itakayowawezesha kufanya kazi.

Pamoja na kuwepo kwa sheria hiyo, mbona bado kuna baadhi ya waajiri hawafuati utaratibu huo, ili kupunguza idadi ya wanaoombaomba mitaani, stendi?

Zile asilimia mbili za mikopo isiyo na riba, inayotolewa na kila Halmashauri kutokana na makusanyo ya mapato ya ndani; tumejiridhisha kwa kiasi gani zimewainua kiuchumi wenye ulemavu?

Iko wapi ripoti ya tathimini ya namna walivyopiga hatua moja kiuchumi au tunafanya siasa?

Kongole kwa Idara ya Sera na Mipango, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, kwa kuamua kuja na mapitio ya sera ya taifa ya huduma kwa watu wenye ulemavu ya mwaka 2004, ili iendane na mazingira ya sasa.

Kwenye suala la ajira, wamekuwa wakibaguliwa jambo ambalo limekuwa likiwaathili kisaikolojia.

Kwa namna iwayo yote ile, serikali imeweka kipaumbele kutoa nafasi za ajira kwa watu wenye ulemavu, ambao wanakidhi vigezo na wenye sifa.

Ndio maana serikali imeweka msisitizo kwa mwombaji kujieleza uleumavu alionao, ili kurahisisha uchambuaji wa maombi ya kazi, lakini suala hili bado limekosa uwazi na kusababisha changamoto kwa baadhi ya waombaji kukosa nafasi.


***• Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI





Ilikuwa siku ya furaha kwa familia ya Mponeja baada ya binti yao kufunga ndoa na Serdar Gormez ambaye ni raia wa Uturuki. Harusi hiyo ilifungwa jijini Mwanza hivi karibini. **PICHA: MC SARAGATA.**





MITINDO

## FULANA NYEMBAMBA

# Vazi la mahaba zaidi

FULANA laini na nyembamba inafahamika kama vazi maalum lenye hisia kali ya mahaba au mapenzi anapovaa mwanaume.

Vazi hili linamfanya mtu kuonyesha misuli na umbo lake halisi, jambo ambalo wanawake wengi huvutiwa nalo pale mwanaume anapovaa.

Ukiangalia kwa umakini unaweza kudhania kwamba ni nguo ya mazoezi, lakini ukweli fulana ya aina hiyo inavaliwa nyakati na mahali popote.

Wataalamu wa mavazi wanasema kwamba wanaume wanaovaa fulana nyembamba mara nyingi huonyesha utanashati na mvuto usio wa kawaida, kuliko mavazi mengine.

Katika chaguo zuri kwa mtu anayetaka kuvaa fulana nyembamba, ni muhimu kuangalia ukubwa, ubora wa kitambaa na ulaini wake.

Vazi hili halina chaguo na nguo zinazoambatana nayo, viatu au mapambo mengine ya mwili.

Hata hivyo, unashauriwa kuvaa na suruali za Jeans, kitambaa au kaptura fupi.

Picha zote na Pinterest









UREMBO



# Alovera hung'arisha ngozi

NGOZI nzuri na yenye kuvutia siyo lazima kutumia vipodozi vyenye kemikali, bali kutumia bidhaa ya asili yenye kuleta afya ya ngozi.

Mafuta ya mshubiri maarufu kama Alovera, ni aina ya bidhaa ambayo inasaidia sana ngozi kuwa nyororo na yenye afya nzuri.

**Faida za Aloe Vera**

Mafuta ya Alovera yana manufaa kwa ngozi iliyopasuka na kavu.

Pia yanasaidia kupambana na baridi kali, kuchomwa au , kuumwa na wadudu, malengelenge na athari ya mzio.

Mafuta ya Alovera hutumiwa kama sehemu ya matibabu ya ngozi na kuifanya ngozi kuwa na afya, kulainisha na kung'arisha.

Jambo la kufurahisha yanaweza kutumika kwenye ngozi kavu kuifanya iwe laini na ya kung'aa.

Alovera huondoa ukurutu, huponyesha haraka vidonda na mmba wa ngozi.

Inasaidia kuondoa seli za ngozi zilizokufa na ina uwezo wa kupenya vizuri na inasafirisha vitu vyenye afya kupitia ngozi.

Pia inasaidia kwa wanaokaa kwenye viyoyozi ngozi kubaki na unyevu nyevu na kuzuia ngozi ya midomo kukatika.

Mafuta haya ni muhimu kwa kuzuia kuzeeka kwa ngozi.

***Picha zote na Pinterest***

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Kripsi inachangamsha mwili





KRIPSI za viazi ni aina ya chakula kinachochangamsha mwili ambacho huliwa wakati wowote.

Wengi wanapenda kula aina hii ya chakula lakini hawajui namna ya kutengeneza kwa ajili ya kula na familia au kuuza ili kujipatia kipato.

**MAHITAJI**

Viazi kiasi unachotaka, mafuta ya kupikia, chumvi au pilipili ya unga, mashine ya kukatia, moto wa mkaa au gesi na vyombo vya kupikia.

**HATUA ZA KUPIKA**

Kwanza menya viazi vyako na viweke kwenye maji ambapo vitaoshwa.

Chukua mashine yako ya kukatia na ioshe na maji kwanza, kisha kata viazi vyako ili viweze kuwa kama vipande vyenye umbo la duara.

Weka mafuta kwenye kikaangio na uweke jikoni na hakikisha moto wako unawaka vizuri.

Hakikisha wakati unakata viazi vyako vidondokee kwenye maji ili visigandane.

Hakikisha mafuta yanapata moto ndio uweke vipande vya viazi vyako humo.

Subiri na kaa muda wa dakika saba hadi 10 kisha geuza na baada ya muda mchache krips zako zitakuwa zimesha iva.

Ipua na uweke kwenye chujio la kuondoa mafuta.

Hakikisha mafuta yanachujwa na krips iwe kavu ili wakati unaweka kwenye vifuko isitengeneze mafuta ndani yake itakera.

Weka kwenye beseni kisha weka chumvi kwa mbali, kabla ya kupepeta ili ichanganyike na iwe tayari kwa kuwekwa kwenye vifuko au kitenga kwenye chombo tayari kwa kuliwa.

Pilipili ya unga pia tunaweka baada ya Kripsi kutoka kwenye kikaango na kupoa.

MAISHA NI NYUMBA

Na Restuta James

# Yatumie vizuri madirisha yako

JE, umewahi kutamani kuwa na sehemu ndogo ya kustarehe, kupata kikombe cha kawaha, glasi ya juisi au kufanya kazi kwenye kompyuta?

Kama unafikiria kujenga nyumba mpya au kukarabati nyumba yako basi zingatia namna ya kutumia madirisha yako kwa kuongeza kitu cha tofauti kitakachokufanya ufurahi uwapo nyumbani kwako.

Wataalamu wa mapambo ya ndani wanaeleza namna bora ya kubuni madirisha ya kisasa yatakayokupa nafasi ya kuongeza nakshi zaidi.

Kwa maeneo yenye joto na mbu kama Dar es Salaam, inashauriwa kuwa mwenye nyumba achague dirisha moja au machache ya kuboresha matumizi.

Mtaalamu Lucy Goldberg, anasema unaweza kujengea kimeza kidogo kwenye dirisha ili kupata nafasi ya kupumzika pale unapohitaji mwanga mwingi hasa kwa wanaotumia kompyuta.

Anasema kama dirisha ni kubwa, ukishajenga meza, badala ya kiti cha kukalia unaweza kuweka kibenchi ambacho kitafaa kulala ikiwa utataka kupumzika eneo hilo.

Anasema unaweza kutumia nafasi hiyo ya dirisha kuweka mito, kitabu upendacho au ua.

"Ni eneo zuri la kufurahia mwanga wa jua na mandhari ya nje," anasema.

Viti vya dirishani vinafaa kutumika kama ofisi yako ya nyumbani.

Inafaa kuwekwa vitu vichache kama kitabu, kompyuta, ua, mto na kikombe au glasi.

Ongeza ukisasa na uzamani kwenye eneo hili, tumia zaidi mbao.







# Weka mfumo imara kuepusha majanga ya moto

USALAMA wa nyumba ni jambo la msingi kuliko vyote katika ustawi wake.

Mbali na vitu vingine ambavyo ni muhimu katika nyumba kuanzia maandalizi, wakati wa ujenzi na baada ya ujenzi, kuweka mfumo mzuri wa kuepusha majanga ya moto.

Msanifu Majengo, Abel Mkaku, anasema zipo njia mbalimbali za kutumia za kukabiliana na majanga ya moto kwenye nyumba na kwamba mojawapo ni kutumia mfumo bora wa umeme ambao msingi husababishwa na hitilafu zinazotokana na mifumo duni ya umeme kwa kuweka vifaa duni wakati wa kuweka umeme kwenye nyumba.

Njia ya pili anasema ni kutumia vizuri soketi na swichi ya umeme pamoja na kuepuka kutumia vifaa vya umeme duni vikiwamo redio, pasi, jokofu, televisheni, jiko na vinginevyo.

"Kutokana na ujenzi duni, si jambo la kustaajabisha kukuta nyumba moja ina soketi moja au mbili. Hili husababisha watu kujaza kila kifaa kwenye soketi hiyo moja, na kusababisha soketi hiyo izidiwe na kuwaka moto," anasema.

Ya tatu, anasema ni kutumia vyema jiko lililoko ndani ya nyumba.

"Jiko lililoko ndani ya nyumba unatakiwa kuchukua tahadhari zaidi. Haijalishi ni jiko la umeme, gesi au mafuta. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ili kuepuka majanga ya moto. Lisafishe, usiliache likiwa na mafuta au kuacha karatasi karibu nalo," anasisitiza.

Njia ya nne, anasema ni kuepuka kuacha moto ukiwaka karibu na nyumba. Anashauri pia kutumia moto ulio wazi kwa uangalifu na kwamba wakati mwingine watu huwasha vibatari, mishumaa au hata sigara ndani ya nyumba.

Kwa mantiki hiyo, anasema ni vyema kuandaa miundombinu na vitu vya kukabiliana na moto.

"Ni vema kuchukua tahadhari kabla ya janga kutokea, ni muhimu ukahakikisha nyumba yako ina miundombinu ya kukabili moto pamoja na vifaa vya kuzimia moto.Weka vifaa vya kuhisi moto au moshi.

"Hakikisha watu wanaweza kujiokoa kwa kupitia madirishani au kwenye milango ikiwa moto utatokea. Yaani jenga madirisha na milango inayoruhusu watu kujiokoa. Weka vifa vya kuzimia moto kama vile mpira wa maji wa kuzimia moto pamoja na mitungi ya hewa," anasema.

Mtaalaamu huyo anashauri usitumie vitu vinavyoshika moto haraka ikiwamo mafuta ya gari, rangi, gesi, pamba.

"Hakikisha unachunguza kila bidhaa unayotaka kuiweka kwenye nyumba yako ili kubaini kama inashika moto haraka ili ihifadhiwe kwa tahadhari kubwa," anashauri.


Jingine analoshauri ni kuchukua tahadhari umeme unapokatika kwa kuzima vifaa vya umeme.

"Tumia vifaa vya kutawala kiwango cha umeme. Hivi huhakikisha umeme unaoingia kwenye vifaa vyako ni wa kiwango kinachotakiwa na huwa na mfumo unaojulikana kama "delay" ambao hauruhusu umeme kuingia kwenye vifaa moja kwa moja mara unaporudi," anasisitiza.





## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
'NINI TENA JAMANIIII?
ZE BOSI
'MIRADI'
NIMEKUPA TALAKA TOKA ULIPONIMALIZIA 'KIINUA MUGONGO' NISHAKUKATAA
KAPUKU
BAR
'VYUPI' NJE NJE! HADI NAONA GIZA!
BONGO FLEVA
SASA BENO UNAFANYA NINI MWANANGU?
ULIHITAJI 'MSUKUMO' ILI UFANYE MAENDELEO
TUSHAKUWA WATU WAZIMA TUACHE MAMBO YA KITOTO!
KWA HIYO KWA WAZAZI WAKO WEWE SIO MTOTO AU SIO?
MBONA LONG'TAIMU NILIKUWA NACHAGUA MINUSO?
NIMECHUNIWA SICHANGII...
KADI
MIALIKO
USWAZ

## HABARI KIMATAIFA




Polisi nchini Bangladesh wakilinda mitaa ya mji mkuu wa nchi hiyo Dhaka, kufuatia maandamano yanayoendelea kupinga serikali. **PICHA: GETTY IMAGES**

# Uganda yaendelea kukana kuwasaidia M23 nchini DRC

**KINSHASA,** DRC

SERIKALI ya Uganda imeendelea kukana kusaidia kundi la waasi la M23 wanaopigana nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kama ripoti ya Umoja wa Mataifa inavyoeleza.

Balozi wa Uganda nchini DRC, Matata Magara, alisema hayo wakati alipoitwa na serikali ya nchi hiyo kuelezea uchunguzi huo uliofanywa na Umoja wa Mataifa.

Tangu mwaka wa 2021, Waasi wa M23 wameripotiwa kuteka maeneo mengi katika jimbo la Kivu Kaskazini, huku ripoti hiyo ikituhumu Uganda kwa kuwaunga mkono kijeshi waasi hao pamoja na kutoa taarifa za kijasusi.

Balozi huyo alikana taarifa kuwa nchi yake ilikuwa inawaunga mkono waasi hao wakati akizungumza na Naibu Waziri wa Mambo ya kigeni wa DRC, Gracia Yamba Kazadi.

"Msimamo wetu umesalia kuwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki tunahitaji kufanya kazi kwa pamoja kuwaondoa watu wanaotusumbua" alisema Magara.

Aidha aligusia oparesheni ya pamoja mashariki ya DRC kati ya wanajeshi wa Congo na wale wa Uganda katika vita dhidi ya waasi wa ADF wanaohusishwa na wapiganaji wa Islamic State. Kundi hilo limekuwa likiripotiwa kutekeleza mauaji ya maelfu ya raia mashariki mwa nchi hiyo.

Kwa mujibu wa Magara, aliitwa na Kazadi akitaka kufahamu kuhusiana na masuala ya uhusiano kati ya mataifa hayo mawili na kutaka kuelewa kinachoendelea.

Katika ripoti iliyochapishwa Julai 8, mwaka huu wataalam wa Umoja wa Mataifa, walithibitisha uwepo wa uungwaji mkono kutoka kwa maofisa wa kijasusi wa Uganda kwa waasi wa M23.

Ripoti hiyo inaeleza karibia wanajeshi 3,000 hadi 4,000 wa Rwanda walikuwa wakipigana pamoja na waasi wa M23 mashariki mwa DRC.

Aidha ripoti ya wataalam hao pia ilieleza kwamba waasi hao walikuwa wanapokea msaada kutoka kwa baadhi ya maofisa wa jeshi la Uganda UPDF.

**RFI**

## Huduma duniani zarejea baada hitilafu kudhibitiwa

**LONDON,** UINGEREZA

HUDUMA katika viwanja vya ndege na biashara katika sehemu mbalimbali duniani zinaendelea kuathirika kutokana na tatizo la teknolojia kuathiri mifumo ya kompyuta kuanzia Alhamisi ya wiki hii.

Biashara za mabenki, hospitali na mashirika ya usafiri ya ndege zilikuwa miongoni mwa zile zilizoathirika baada ya kampuni ya usalama mtandaoni CrowdStrike kutelekeza programu mpya iliyokuwa na hitilafu na ambayo iliathiri programu zinazotumia Microsoft Windows.

Mkuu wa kampuni ya CrowdStrike aliomba msamaha kwa hitilafu hiyo na kusema kwamba imerekebishwa, lakini alikiri kwamba itachukua muda kabla ya programu zote kufanya kazi vizuri bila matatizo.

Hata hivyo baadhi ya huduma za mashirika ya ndege zilitarajiwa kurejea utoaji huduma kama kawaida baada ya maelfu ya safari kusitishwa.

Mashirika hayo yanasema huenda changamoto za kucheleweshwa na kufutwa kwa safari zikaendelea kushuhudiwa wiki nzima.

Biashara nyingi sasa ziko mbioni kutimiza maagizo ya wateja na huenda shughuli hiyo ikachukua siku kadhaa. Huduma za afya nchini Uingereza, Israel na Ujerumani pia zilikumbwa na matatizo, na baadhi ya huduma zilisimamishwa.

Hitilafu hiyo iliyoshuhudiwa duniani kote ilizua wasiwasi kuhusu mfumo na udhabiti wa mtandao wa teknolojia duniani kote, na jinsi hitilafu katika mfumo mmoja inaweza kuwa na athari kubwa kiasi hicho katika sekta mbalimbali.

Tatizo lilianza Alhamisi majira ya 1:usiku, likiathiri watumiaji wa programu ya Windows inayotumia mfumo wa usalama mtandaoni wa CrowdStrike Falcon. Kampuni ya Microsoft ilisema ukubwa wa tatizo lilidhihirika Ijumaa asubuhi.

Hata hivyo, kufikia Ijumaa jioni, changamoto hiyo ilikuwa imeshughulikiwa katika sehemu nyingi duniani, huku viwanja vingi vya ndege vilisema japo kulikuwa na matatizo katika mifumo ya malipo ya wateja, safari nyingi za ndege zilianza.

**BBC**

## Marekani inahofia Iran urutubishaji wa nyuklia

**WASHINGTON,** MAREKANI

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken, amesema Iran ina uwezo wa kutengeneza nyenzo za malighafi zenye kufanikisha utengenezaji wa silaha za nyuklia ndani ya wiki moja au mbili.

Habari hizo kuhusu uwezo wa Iran zilitolewa baada ya uchaguzi wa hivi karibuni uliomuingiza madarakani Rais Masoud Pezeshkian.

Rais Pezeshkian aliahidi kuiondoa Iran katika hali ya kutengwa na kufufua mazungumzo ya nyuklia kati ya Iran na mataifa yenye nguvu duniani.

Blinken alisema kile walichokishuhudia wiki iliyopita na miezi kadhaa ni kitendo cha nchi hiyo kuendelea na mpango wake wa nyuklia.

Mwaka 2018, Marekani ilijiondoa katika mpango wa nyuklia, ambao uliundwa katika namna ya kudhibiti mwenendo wa matumizi ya nishati ya atomiki wa Iran, kwa makubaliano ya jumuiya ya kimataifa kuliondolea taifa hilo vikwazo.

**DW**

# Biden ang'ang'ania kugombea urais

**WASHINGTON,** MAREKANI

Rais wa Marekani, Joe Biden, anatarajia kurudi katika kampeni zake wiki inayokuja, wakati shinikizo kali kutoka kwa wanachama wa Democratic ambao wanamtaka kujiuzulu nafasi yake ya mgombea mteule.

Hata hivyo, Biden hajaonyesha nia ya kujiuzulu, akisisitiza Ujumaa wanachama zaidi wa Democrat walijitokeza wakimtaka ajiuzulu ili kukifanikisha chama hicho kupata ushindi.

"Dau ni kubwa, na chaguo ni wazi. Kwa pamoja tutashinda," alisema Biden akimaanisha bado ataendelea na mbio zake.

Kauli hiyo ilionekana kujibu ripoti zinazokinzana kwamba wandani wa Biden wanajadili mustakabali wa rais huyo anayekabiliwa na changamoto za kiafya iwapo atasalia kwenye kinyang'anyiro hicho au la. Katika wiki kadhaa zilizopita, kiongozi mwenye umri wa miaka 81, amekumbwa na shinikizo la kisiasa kumtaka ajiuzulu.

Baadhi ya watu waliotoa wito huo ni viongozi ndani ya chama chake ambao walimuhimiza ajiondoe kwenye kinyang'anyiro.

Madai ya wanachama hao wanajikita hasa kupoteza wafadhili wakuu na shinikizo la uamuzi wake wa kugombea kiti hicho unaweza kukigharimu chama hicho.

Wanademocrat wana udhibiti wa bunge la Congress.

Angalau wabunge 12 wa chama cha Democratic wamemtaka akae kando siku ya Ijumaa pekee.

Makamu wa Rais Kamala Harris ambaye anaangaliwa kama chaguo kuu la nafasi ya Biden alipewa jukumu la kuwafariji wafadhili waliokuwa na wasiwasi kwa kuongea nao kwa simu alfajiri ya Ijumaa.

**BBC**

MAKALA

# MNAOHAMA VYAMA WEKENI AKIBA, KESHO NI NDEFU



Na Magabilo Masambu

**Wamejenga hako kautamaduni mwisho wa siku ikawa ndiyo tabia na hutawasikia mahala popote wakisemana vibaya. Hapa naikumbuka kauli ya aliyekuwa Waziri Mkuu Edward Lowassa (marehemu). Aliporejea CCM akitoka CHADEMA alikokwenda kugombea urais mwaka 2015, alisema maneno machache tu kwamba**

UKICHUNGUZA vizuri siasa hasa za kiafrika, unaweza kushindwa kabisa kuelewa nia ya wanasiasa wengi. Jambo hili limefanya siasa kuwa sehemu ya maigizo huku ikiwa imebeba mstakabali wa maisha ya watu.

Leo kumwaminisha mtu mwenye akili timamu kwamba siasa si maigizo na wala si mchezo mchafu kama ambavyo imekuwa ikiitwa ni vigumu sana.

Siasa ya kweli ni kama dini kwa maana ya kuwa na imani ya yale yaliyokufanya ukaingia kwenye dini hiyo.

Mtu anapoamua kwamba sasa mimi ni dini hii lazima awe amejiridhisha juu ya imani yako na kwamba hutafanya watu waone kama ni sehemu ya maigizo.

Tangu awamu ya tano ya uongozi wa nchi yetu, kumekuwa na wimbi kubwa la watu kuhamahama vyama japo hata miaka ya nyuma walikuwapo kina Augustino Lyatonga Mrema waliohama wengi wakitokea Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kutimkia vyama vya upinzani.

Ilikuwa iwe hivyo kwa sababu vyama vingine karibu vyote vilipoanzishwa vilianzishwa huku CCM ikwa tayari safarini.

Hoja yangu si kuhama kwa sababu wanaohama wana haki hiyo kikatiba lakini kinachonishangaza na pengine kinawashangaza wengi ni yale wanayoyazungumza baada ya kuhama chama A kwenda chama B. Tabia hii ya kutokuweka akiba ya kesho hujitokeza sana kwa wanasiasa wanaohama upinzani kwenda chama tawala.

Wale wanaohama chama tawala kwenda upinzani, wengi wao huwa wanazungumza kwa tahadhali huku wakitafakari, hivyo kuweka akiba ya kesho kwa sababu wanajua kesho yao ni ndefu lolote linaweza kutokea.

Nimewahi kusema mahali kwamba ikiwa umeoa mwanamke au umeolewa na mwanamume, mkishaachana na ukaanzisha uhusiano mwingine, kumsema vibaya uliyeachana naye haitakusaidia hata kidogo kujenga uhusiano mpya zaidi uliye naye sasa.

Atajua kwamba siku mkiachana utamsema vivyo hivyo kwa utakayempata mpya jambo litakalomfanya aishi na wewe kwa tahadhari kubwa.

Wahenga wanasema anayekwambia habari za watu wengine pia huwa anawaambia habari zako. Hii ni kwa sababu, tabia ni kama ngozi unaweza kulazimisha kuibadili ukajikuta inabaki na mabaka kama sare za jeshi la wananchi.

Uhakika nilio nao ni kwamba wengi wa aina hiyo ya wanasiasa huwa wanakuwa na ujasiri wa kusema hadharani, lakini wanaporudi nyumbani na kupata muda wa kutafakari walikotolewa, ambako mtu mmoja amewahi kupaita jalalani, huwa wanalia sana wakiwa peke yao pindi wanapopiga picha hali za maisha walizo kuwa nazo, mpaka wamekuja kuonekana watu wa maana na sasa wanaonekana kupendwa.

Kuna wakati unatumiwa kama fimbo kwa sababu wanazijua akili zako zilivyo. Wakati unatukana na kusema vibaya wao wanakonyezana na kunong'onezana juu ya uelewa wako na kwa sababu wameshakujua, hawatakushtua maana wao huwa si tabia zao na wanafundishana kwamba, hata ikitokea ukaona hapa hapakufai, basi ukiamua kuchukua uamzi wowote wa kuachana nasisi basi ukomo wa mazungumzo yako utakuwa hapa mpaka pale.

Wamejenga hako kautamaduni mwisho wa siku ikawa ndiyo tabia na hutawasikia mahala popote wakisemana vibaya.

Hapa naikumbuka kauli ya aliyekuwa Waziri Mkuu Edward Lowassa (marehemu). Aliporejea CCM akitoka CHADEMA alikokwenda kugombea urais mwaka 2015, alisema maneno machache tu kwamba "narudi nyumbani nisiulizwe kwanini nimerudi, narudi nyumbani." Wanasiasa wengine pia wanatakiwa kuiga haya.

Katika siasa, suala la nyakati na vizazi ni la kuwa nalo makini sana wakati wa kuzungumza popote kuhusu siasa na wanasiasa.

Kuna maneno yalikuwa yakizungumzwa kipindi fulani yalileta matokeo mazuri kisiasa, lakini maneno hayovhayo ukiyazungumza nyakati za leo, wewe ndiwe unaweza kugeuka kituko na watu wakakushangaa.

Nadhani hawa watu wanaohamahama kila siku, wapewe muda mrefu wa kushiriki kujenga vyama bila kupata nafasi yoyote ndani ya vyama wanavyohamia kwa sababu kupata kwao nafasi za madaraka au kugombea wakati mwingine kunavunja mioyo ya wale ambao wamekaa muda mrefu huko kwenye vyama vyao wakingoja.

Hawa wanaohama wana malengo yao, mojawapo ni kujipatia nafasi walizozikosa kule walikokuwa. Pia ni muhimu kutazama hilo, watu wanaweza kuonyesha sura za furaha machoni lakini kimoyomoyo wanaumia kuona wahamiaji wanapata nafasi za kugombea halafu waliopambana wakikaa kwenye foleni.

Ushauri wangu, hakuna sababu ya kutukana na kusema vibaya juu ya watu wengine, kuna maisha nje ya siasa lakini zaidi, kumbukeni nyakati mlipokuwa mnaonekana wazee wakati ni vijana na sasa ni wazee lakini mnaonekana kama vijana.

**0689157789**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Nilidhani wifi kumbe mke mwenzangu*



Na Adam Fungamwango

**Mwanamke akajifanya ametoka kijijini akaja kwa mpenzi wake, akapokewa na mama mwenye nyumba. Wakaishi kwa muda mrefu kama mtu na wifi yake. Ukweli haikuwa hivyo. Walikuwa mtu na mke mwenzake. Siku mke alipokuja kujua 'kulichimbika'. Hebu tutembee na mashairi ya wimbo huo.**

KWENYE maisha ya ndoa, kuna mambo mengi sana, hivyo yeyote anayetaka kuingia huko anapaswa ayafahamu kwanza kabla ya kuingia katika taasisi hiyo, ili kukabiliana nayo.

Mara nyingi uvumilivu ndio unaotakiwa ili kuvuka hapo. Ukiona wanandoa wamekaa miaka 30 mpaka 50 ndani ya ndoa yao, si kwamba ilikuwa na raha tu. Walipitia changamoto nyingi sana lakini walikuwa wavumilivu, wakakaa chini kuyasuluhisha na wakavuka salama.

Wengi waliodhania ukioa tu au kuolewa, basi unakuwa kama dunia yote yako na hakuna changamoto zozote utakazokutana nazo, ndio wanaokuwa na kipindi kifupi tu kwenye ndoa kabla ya kunyoosha mikono juu, yaani kuachana.

Vijana Jazz Band waliimba wimbo mmoja uitwao 'Tamu na Chungu ya Ndoa'. Una maneno yafuatayo;-

"Ndoa una tamu na chungu ulielewe hilo mpenzi wangu wewe. Tutakapooana tutafanya sherehe nyingi, lakini kumbuka maisha ya ndoa, yana tabu na raha, aa yaya, tusiyafuate maneno ya pembeni, yataharibu bure ndoa yako.

Uvumilivu kwenye ndoa ni muhimu, hakuna ndoa inayokosa misukosuko."

Wimbo huu umemaliza kila kitu. Ila sasa nataka nikupe kisa kimoja kilichotokea kwenye ndoa moja ambacho kimesimuliwa na bendi ya Tancut Almasi Orchestra.

Wimbo huo ulitungwa na Kyanga Songa unaitwa 'Nimemkaribisha Nyoka'. Unaelezea moja ya matatizo yanayoweza kutokea kwenye ndoa.

Ni kisa cha kusikitisha sana. Kinaeleza juu ya mwanaume mmoja aliyekuwa na mpenzi wake nje ya ndoa. Akaona haitoshi. Akataka kumpeleka kabisa nyumbani kwake kwa mkewe. Akapiga plani zake, akishirikiana na mpenzi wake wakaamua kuitana mtu na dada yake.

Mwanamke akajifanya ametoka kijijini akaja kwa mpenzi wake, akapokewa na mama mwenye nyumba. Wakaishi kwa muda mrefu kama mtu na wifi yake. Ukweli haikuwa hivyo. Walikuwa mtu na mke mwenzake. Siku mke alipokuja kujua 'kulichimbika'. Hebu tutembee na mashairi ya wimbo huo.

"Nimepatwa na mgeni nyumbani kwangu, mume wangu hakuwepo alikuwa kazini, mgeni akajitambulisha ya kwamba yeye ni dada wa mume wangu, na kwamba anatokea nyumbani, kwa wazazi wake kijijini. Nikamkaribisha bila shaka yoyote mama, nikampikia chai na chakula nikampa wifi yangu."

Plani iliyopangwa ni hiyo, mtu aliyeanza kwenda nyumbani hapo ni yule hawara. Mwanamume yeye alijifanya kama hajui kitu. Na wala hakumwambia mkewe kuwa dada yake atamtembelea. Wimbo unaendelea.

"Mume wangu alipotoka kazini nikamweleza mambo yote mama hee, naye akakubali kwamba ni dada yake ambaye wamezaliwa tumbo moja lele, basi tukaendelea kuishi kama vile mtu na wifi yake ndani ya nyumba, bila matatizo yoyote mama hee."

Jamaa alivyorudi kutoka kazini alijifanya hajui chochote, akamkuta tu mgeni, wimbo haukueleza, lakini ikaonekana alipofika na kumkuta akasema "Waoo dada umekuja, habari za kijijini." Hii ni kuongeza uzito mke akubali kama ni dada yake. Wimbo unaendelea.

"Aaaaa, kumbe nilikuwa nakula na nyoka sikujua, aaaa, kumbe nilikuwa nakula na nyoka sikujua."

Jinsi wimbo huu unavyoimbwa, inaonekana ni kwamba tukio limeshafanyika na mke anasimulia mkasa uliompata, ndiyo maana anasema kumbe alikuwa anakula na nyoka ila hakujua. Mwishoni anajuta kwa kusema kumbe alikuwa amemkaribisha nyoka

"Nimemkaribisha nyoka eee, kumbe nimemkaribisha nyoka eee, Salima nilidhania wifi yangu, kumbe ni mke mwenzangu mama."

Hapa mwishoni tunapata jina la mwanamke huyo fedhuli aliyekwenda nyumbani kwa mwenzake na kuitikisa ndoa ya mwenzake, anaitwa Salima.

Hii na mingine ni mikasa inayojitokeza sana kwenye jamii, ambayo wanamuziki wa zamani wamekuwa wakisimulia kwa njia ya kuhabarisha, kuburudisha na kuelemisha pia.

Haya mambo si lazima yatokee kwenye ndoa na wengine hayatowatokea kabisa, lakini kwa uchache visa kama hivi vipo na ni moja kati ya changamoto nyingi kwenye ndoa zinazowapata wote wawili, mke na mume. Visa vipo vingi sana, leo nimeweka hiki kimoja, nitaendelea kuwaletea visa vingi kwenye ndoa vilivyoimbwa na wanamuziki wa dansi nchini Tanzania.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Aka Simtaki-3

BAADA ya kumaliza masomo yake ya kidato nne na kushindwa kuendelea na masomo kutokana na hali duni ya wazazi wake, Shani alitakiwa kuolewa. Akakubali, lakini ni kwa yule ambaye anampenda. Haikuwa hivyo, kwani baba yake mzee Chilambo alimlazimisha aolewe na mwanamume mwenye uwezo, mali na fedha ili asiende kuteseka. Tatizo likaanzia hapo, mwenye pesa hakupendwa na Shani, asiye na uwezo alikuwa kwenye moyo wake. Baba anamtaka mwenye uwezo. Jambo hili linazua mgogoro mkubwa kwenye familia tatu, za binti na wachumba wawili. Nini kitatokea. Usikose kila nakala ya gazeti hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

PAMOJA na tabia yake ya kutembea na wanawake wengi, lakini moyo wake uliangukia kwa Nyendo.

Fotu aligonga mwamba kwa binti huyo, licha kumpa zawadi mbalimbali, kumhonga pesa ambazo alikuwa akizikubali, lakini hakufanikiwa kuwa naye. Mwishowe alianza vitisho kwa msichana huyo ambaye aliamua kukimbilia polisi. Kitendo cha yeye kuitwa polisi na kuonywa mbele ya wazazi wake na wa Nyendo kulimfanya anyong'onyee. Hata hivyo moyo wake uliendelea kuwa kwake. Kwa muda mfupi tu akaacha mbwembwe zake zote, kuchukua ovyo wasichana, badala yake aligeuka kuwa mnyonge, aliyependa kukaa peke yake na kukaa kimya.

Hali hiyo iliwatisha wazazi na baadhi ya rafiki zake wachache, mwisho aliwatuma kwenda kwa Nyendo wambembelezee akubali kuwa wake na kuahidi kumuoa.

Jibu lililotoka kwa msichana huyo ni kwamba amekubali, lakini kwa sharti ya kutokuwa na uhusiano wowote wa kimapenzi mpaka watakapofunga ndoa.

Hapo ndipo ugomvi ulipomalizika na wakawa wanakutana na kuzungumza, kila mmoja akiahidi kuwa mwangalifu mpaka pale watakapotimiza ahadi.

Ingawa hakuna yoyote aliyekwenda kumwambia mzazi wake, lakini tetesi zilianza kuenea kijijini hapo kuwa Fotu anataka kumuoa Nyendo.


"Umempata mwingine!!?" Akashangaa Kibwana na kulirudia neno lililotakwa na Fotu.

"Sikiliza Kibwana, katika pitapita zangu jana mchana kwenye kijiji cha mbele hapo Lalangulu, nimekutana na msichana mmoja bomba sana! Yaani ni mzuri. Nikisema mzuri nina maana ya uzuri. Na inaonekana anatoka katika familia fukara, yule msichana akimpata mwanaume kama mimi ninayetoka kwa wazazi wanaojiweza kudogo, atakuwa kama malkia!"

Maneno yale yalimshangaza sana Kibwana. Akamtazama Fotu kwa mshangao, halafu akamuuliza.

"Ni wewe kweli unayesema maneno haya? Ni Fotu yule yule ninayemfahamu? Yule ualiyekuwa unampenda kwa dhati Nyendo. Tuliyekushuhudia unalia machozi kwa mara ya kwanza kwa ajili yake?"

"Hizo sasa ni ngonjera unaleta Kibwana. Mimi nataka kumuoa yule niliyemuona kule Lalangulu." Akaongea kwa msisitizo kiasi cha Kibwana kugundua kuwa rafiki yake hatanii.




**"Ni wewe kweli unayesema maneno haya? Ni Fotu yule yule ninayemfahamu? Yule ualiyekuwa unampenda kwa dhati Nyendo. Tuliyekushuhudia unalia machozi kwa mara ya kwanza kwa ajili yake?"**

"Dah!" Akashangaa Kibwana, halafu akamuuliza. "Umeshaongea naye kuhusu suala hilo?" "Hapana, nilivyomuona tu roho ilinilipuka, kusema kweli yule msichana aliinishtua moyo wangu. Haya yeye mwenyewe alitambua hilo, maana aligeuka ananitazama halafu akatabasamu."

"Hukumwita labda mkazungumza kitu chochote?" "Hapana, mimi nilisimama, yeye akawa anatembea kwa madaha, akapita mbele yangu, nikageuka kumtazama na yeye mbele akageuka na kunitazama, kusema kweli hadi nimpate yule msichana." "Umpate kwa kumchezea tu kama kawaida yako, au umuoe?" Kibwana alizidi kumminikia maswali rafiki wake mithili ya askari polisi.

"We!!! Yule nataka nimuoe kabisa, sitaki utani kama kuna mtu anaweza kwenda kwao hata kesho aende tu, mimi nitampa barua anipelekee." "Mmmh! Hapana mimi unaisamehe tafuta mtu mwingine wa kupeleka, siwezi kufanya kazi hiyo nikaonekana mnafiki. Tumekubembelezea Nyendo, tumeenda mpaka kwao, leo hii ionekane napeleka barua kwingine! Yeye na wazazi wake watanionaje?" "Hilo halina neno, nitatafuta mzee mmoja mwenye busara zake aende." Fotu, mzee mwenye busara kwenye kijiji hiki hawezi kukubali kwa sababu kila mmoja anajua barua ya posa itapelekwa kwa nyendo." "Okay, nitamtafuta hata kwenye kijiji kile kile cha Lalangulu." "Haya, wewe unasema utapeleka barua, una uhakika kama yeye hata mchumba? Au kwenye kijiji kile hakuna mpenzi wake wanaopendana na anataka kumuoa?" Maswali ya Kibwana yalikuwa mengi na kuanza kumchosha Fotu. "Unasikia Kibwana, hilo mimi halinihusu." Akaongea kwa hasira kidogo. "Mimi nataka kumuoa, nitapeleka posa, na nakuhakikishia nitafanikiwa hata kama wewe hutaki, maana maswali yako yanaonyesha kama hupendelei hili nililolifanya. Katika dunia hii pesa ndiyo kila kitu, wazazi wangu wana uwezo, hata ama ana wachumba wanne, nitahakikisha nawapiku kwa nguvu ya pesa. Hiyo ndiyo kila kitu, penye udhia penyeza rupia na pesa inavunja bonde na milima."

**********************************

"Shukuru nimesikia habari zako. Hongera rafiki yangu!" "Hongera ya nini Pembe mbona unanitisha?"

"Nasikia unataka kumposa binti Chilambo?" "Nani?" Shukuru akauliza kama hamfahamu.

"Aaaaah! kwani mzee Chilambo ana mabinti wangapi? Si Shani tu." Mhh! Watu wa kijiji hiki mmezidi umbea, yaani kitu cha siri hiki mmeshakijua!!" "Kwani hilo ni jambo baya la kuficha kweli? Mbona la heri tu." Shukuru alinyamaza kwa muda kama mtu anayetafakari, halafu akatabasamu.

"Ni kweli rafiki yangu nina mpango huo, ila sijui kama utafanikiwa!" "Kwa nini usifanikiwe wakati jambo la heri hili?" "We yule mzee si unamfahamu, au unajizima data." "Nafahamu, kila mmoja anajua ukorofi wake, lakini kwa jambo hili nalo ataleta shida?" "Pembe tatizo huu ufukara nilionao ndiyo wasiwasi wangu. Unajua yule mzee siyo masikini sana, ana kajiuwezo kidogo, sasa ana nyodo sana, na ule ukorofi wake ndiyo kabisa. Ndiyo maana mimi naogopa sasa." "Usiogope Shukuru, kwani umeshaongea na Shani mwenyewe?"

"Mwenyewe hata neno, mimi nimeshaongea naye. Yule ni wangu, sema tuliahidiana mpaka akimaliza shule kidato cha sita, lakini hakufanikiwa kupasua, na wazazi wameshindwa kumuendeleza, nikamuuliza sasa ahadi yetu vipi, akasema wewe tu, siku ukiwa tayari lete barua." Pembe akaangua kicheko kifupi, halafu akamwambia, "sasa wasiwasi nini, mtoto mwenyewe kumbe kafa kaoza." Shukuru akamtazama rafiki yake, halafu akaguna. "Natabiri kama kutakuwa na tatizo." "Haya tutaona.

Siku tatu baadaye Shukuru na mpenzi wake Shani walikutana karibuni na kisima cha kijiji. Hata hivyo, ilibidi waingie nadni kidogo ya pori ili wasije kuonekana na watu wengine wakiwa kwenye maongezi yao nyeti.

"Vipi kuhusu barua?" Lilikuwa swali la Shani kwenda kwa mwenzake. "Hilo ondoa shaka, ila sasa sina pesa ya kufanya sherehe." Shani alimtazama mpenzi wake, halafu akamwambia, "sawa, kuhusu sherehe na mahari nitaongea na mama ili ambebeleze baba, wewe tafuta pesa ya barua tu." "Sawa nimekuelewa." "Usiseme sawa tu nimekuelewa, fanya haraka nahisi kama kuna barua zinataka kuletwa nyumbani." "Kwa nini unahisi hivyo?" Akauliza Shukuru. "Tayari nimeshaanza kuambiwa mambo ya kuolewa. Nimeulizwa kama uatatokea mchumba nitakubali kuolewa? Nikawajibu yule ambaye nitampenda.

Hapo nikaona kabisa kuna kitu." "Sawa Shani, nitawahisha barua. Ila namuhofia baba yako!" "Baba asikutie presha, najua kutakuwa na changamoto kidogo, lakini mimi ndiye mtetezi wako. Mimi ndiye nitayaeolewa.

Mimi ndiyo nitakaa na mume. Sasa haiwezekani mtu anichagulie. Nataka nikae na mwanaume ambaye moyo wangu umeridhia. Siyo wa kulazimishwa." "Ambaye ni nani?" Shukuru akauliza kwa utani." "Una wazimu wewe!" Shani naye akajibu kwa utani pia. Wakagongesheana mikono kwa furaha. Wakacheka na kukumbatiana.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# SIDIKA KUWAPOZA KIMAHABA GEN Z

MPAMBAJI wa video za muziki kutoka nchini Kenya, Vera Sidika, amesema vijana wengi wa Gen Z, wamemtumia ujumbe wa kumtaka kimapenzi na kuwakumbusha kuwa akirudi nchini humo atawafikiria.

Kupitia instastory yake, Sidika amesema vijana hao walitaka kupewa fursa ya kuwa nao katika uhusiano, lakini ameshindwa kukubali kutokana na kuwa yuko nje ya nchi.

"Kusema ukweli sijasahau stori ya Gen Z. kwa vile niko mbali na nyumbani. Uhusiano wa mbali siwezi, wakati nitakapotua Kenya, tutaendelea pale tulikoachia," aliandika Sidika.


# *Blagbonez kaja na 'Fire On Me'*

STAA wa muziki kutoka Nigeria, Akumefule Chukwuemeka, maarufu kama Blaqbonez, ameachia ngoma yake mpya inayoitwa 'Fire On Me'.

Msanii huyo ambaye amepata mafanikio katika albamy yake "Emeka Must Shine" amewapagawisha mashabiki wake baada ya wimbo huo kuvuta hisia zao.

Blaqbonez anafanya vizuri katika majukwaa ya muziki ya kidijitali ameshika nafasi ya kwanza kwenye mtandao wa Apple kwa wiki tatu mfululizo.





# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LIVERPOOL YAMTAKA GUEHI

MARC Guehi anasakwa na Liverpool, ambao wameanza mazungumzo ya kumsajili beki huyo wa kati wa Crystal Palace na England mwenye umri wa miaka 24. ***(Fabrizio Romano)***

### WHARTON AWAKATALIA CITY

KIUNGO wa kati wa England, Adam Wharton mwenye umri wa miaka 20, amekataa ofa kutoka Manchester City, Bayern Munich na Real Madrid ili kusalia Crystal Palace. ***(Sun)***

### MERINO AWANIWA ARSENAL

ARSENAL inapigiwa upatu kuishinda Aston Villa katika harakati za kumnunua kiungo wa kati wa Real Sociedad na Hispania, Mikel Merino mwenye umri wa miaka 28 msimu huu. ***(Mundo Deportivo)***

### SETFORD SAFI KUTUA ARSENAL

ARSENAL imefikia makubaliano ya kumsajili mlinda lango wa kimataifa wa England, Tommy Setford mwenye umri wa miaka 18 kutoka Ajax. ***(Athletic)***

### AHMEDHODZIC AWANIWA

KLABU ya Wolves inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumnunua mlinzi wa Sheffield United mwenye thamani ya pauni milioni 20, Anel Ahmedhodzic mwenye umri wa miaka 25, kuchukua nafasi ya Muingereza Max Kilman aliyejiunga na West Ham. ***(Sun)***

### ALVAREZ ATAKIWA PSG

KLABU ya Manchester City itafanya mazungumzo na mchezaji wao wa kimataifa wa Argentina, Julian Alvarez mwenye umri wa miaka 24, baada ya Copa America. PSG wanavutiwa na mshambuliaji huyo ambaye anataka muda zaidi wa kucheza, lakini City wanataka kusalia naye. ***(Fabrizio Romano)***

### TERLAND AWANIWA MAN UTD

KLABU ya Manchester United iko tayari kumsajili mshambuliaji wa Norway, Elisabeth Terland kutoka Brighton mwenye umri wa miaka 23. ***(Guardian)***

### JAKUB KURUHUSIWA ARSENAL

MCHEZAJI Jakub Kiwior ataruhusiwa kuondoka Arsenal msimu huu wa majira ya joto na beki huyo wa Poland mwenye umri wa miaka 24 anavutiwa na klabu za Serie A. ***(Football Insider)***


### INACIO AWINDWA LIVERPOOL

LIVERPOOL wamemweka mlinzi wa kati wa Sporting Lisbon na Ureno, Goncalo Inacio mwenye miaka 22 kuwa mlengwa wao mkuu katika kipindi cha uhamisho. ***(CaughtOffside)***

### KOOPMEINERS ANYATIWA

JUVENTUS wanamtaka kiungo wa kati wa Atalanta, Mholanzi Teun Koopmeiners mwenye umri wa miaka 26 ambaye pia amekuwa akihusishwa na Liverpool. ***(Rudy Galetti)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MORATA ATUA RASMI AC MILAN

**MILAN,** Italia

ALVARO Morata amejiunga na AC Milan kwa uhamisho wa kudumu kutoka Atletico Madrid, timu hiyo ya Serie A imetangaza.

**Morata, ambaye alikuwa nahodha wa Hispania na kutwaa ubingwa wa Euro 2024, alifanyiwa uchunguzi wa kimatibabu kabla ya kusaini mkataba wa miaka minne na Rossoneri hao.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 alifunga mabao 46 katika mechi 117 akiwa na Atlético baada ya kujiunga na klabu hiyo kwa mkataba wa mkopo wa awali kutoka Chelsea Januari mwaka 2019.

Uamuzi wake wa kuondoka Rojiblancos ikiwa imesalia miaka miwili kumalizika kwa mkataba wake uliwashangaza mashabiki ikizingatiwa kuwa wiki chache zilizopita,

## ●●● Nahodha huyo wa Hispania amejiunga na timu hiyo kwa uhamisho wa...

Morata alikuwa amechapisha picha kwenye Instagram yake akiwa amevalia jezi ya Atlético yenye ujumbe: "Siwezi kufikiria ni lazima iweje kama kushinda na jezi hii na sitaacha hadi nipate kitu na Atletico de Madrid."

Hata hivyo, Morata alikuwa amelalamika wakati wa michuano ya Ulaya nchini Ujerumani kwamba hakupata heshima kutoka kwa vyombo vya habari na mashabiki nchini Hispania.

Juu ya kile kilichomfanya aamue kujiunga na AC Milan, aliiambia Sky Italia: "Jambo rahisi. Uaminifu nilioonyeshwa.

"Najua bado nina miaka bora zaidi ya maisha yangu mbele yangu na ninataka kwenda kwa klabu hii kubwa ambayo ni Milan.

"Ukweli ni kwamba Waitaliano wamenitendea kwa heshima ya ajabu. Siwezi kusubiri kwenda kucheza huko tena.

"Wamenitumia vitu vyote vyema."

Morata aliona muda wake wa kucheza ukipunguzwa mwaka huu lakini akiwa Milan, anatarajiwa kupata dakika nyingi kufuatia kuondoka kwa fowadi Mfaransa Olivier Giroud.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 alihamia LAFC baada ya mkataba wake na Rossoneri kumalizika Juni.

Milan walitangaza katika taarifa yao kwamba Morata atavaa jezi namba 7 katika klabu hiyo.

## HABARI MICHEZO



# N'GOLO KANTE KUTUA WEST HAM UNITED

**LONDON,** England

WEST Ham United ina nia ya kumrejesha kiungo wa kati wa zamani wa Leicester City na Chelsea N'Golo Kante kwenye Ligi Kuu England, kwa mujibu wa ripoti.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 alihamia Saudi Arabia msimu uliopita wa majira ya joto kujiunga na Al Ittihad kwa mkataba wa miaka minne, akijiunga pamoja na Karim Benzema na Neymar.

Katika kilele chake, Kante alikuwa kiungo bora zaidi wa ulinzi duniani, alichangia kwa kiasi kikubwa katika mafanikio ya kushangaza ya Leicester City iliipotwaa ubingwa wa Ligi Kuu England mwaka 2016.

Uwezo wake ulitambuliwa haraka na Chelsea, ambao walishinda taji hilo katika msimu wa kwanza wa Mfaransa huyo Stamford Bridge kabla ya kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi ya Europa na Kombe la klabubingwa duniani.

Matatizo ya jeraha yalimfanya Kante kucheza mechi saba pekee za Ligi Kuu England katika mwaka wake wa mwisho akiwa Chelsea, lakini alitazama nyuma hadi kufikia kiwango bora zaidi kwenye michuano ya Euro 2024 akicheza nafasi ya juu katika safu ya kiungo wakati Ufaransa ilipotinga nusu fainali ya michuano hiyo.

Gazeti la The Guardian limeripoti kuwa West Ham iko kwenye mazungumzo na kambi ya Kante kuhusu kurejea Uingereza na inasemekana kuna utayari kutoka kwa pande zote mbili kufanya makubaliano.

Ada ya pauni milioni 20 imetolewa, huku kocha mpya wa West Ham, Julen Lopetegui akiaminika kuwa shabiki mkubwa wa Kante tangu enzi zake kama kocha wa Real Madrid, na mchezaji mwenyewe alidokeza kabla ya Euro 2024 kwamba kurejea Ulaya kunawezekana.



# Osimhen atakiwa kujiunga PSG

**PARIS,** Ufaransa

WINGA wa zamani wa Nigeria 'Super Eagles', Emmanuel Amunike, amemtaka Victor Osimhen kwenda kujiunga na klabu ya PSG.

Mabingwa wa Ligue 1, PSG kwa sasa wanafanyia kazi mchakato wa kumsajili Osimhen msimu huu wa majira ya joto.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria ana kipengele cha kuachiliwa kwa pauni milioni 130 katika mkataba wake.

Amunike, ambaye alimpa Osimhen mafanikio kimataifa alipokuwa katika timu ya taifa ya chini ya umri wa miaka 17, amesema kuhamia PSG kutasaidia maisha ya mshambuliaji huyo.

"PSG ni timu kubwa inayocheza Ligi ya Mabingwa Ulaya, itakuwa jambo la kufurahisha na jema akihamia huko," alisema Amunike.

# Olmo awa lulu Ulaya

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeungana na Barcelona, Bayern Munich na wapinzani wao Manchester City katika mbio za kuwania saini ya Dani Olmo kutoka RB Leipzig, ripoti kutoka Hispania imedai.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 amekuwa akitawala vichwa vya habari katika ulimwengu wa soka tangu mwezi uliopita kwa kiasi kikubwa kutokana na uchezaji wake akiwa na Hispania wakati wa michuano ya mafanikio kwao ya Euro 2024, ambapo alichangia mabao matatu na pasi mbili za mabao katika kampeni yao ya kutwaa ubingwa.

Mbali na eneo la kimataifa, Olmo amedokezwa kutafuta klabu mpya msimu huu wa majira ya joto.

Kipengele cha kutolewa cha pauni milioni 50.5 katika mkataba wake kinamalizika Julai 20, lakini Leipzig wanasemekana kuwa wanaweza kumuuza hata baada ya tarehe hiyo kupita. AS imearipoti kwamba United sasa inashinikiza kuwasili kwa Olmo huku ujenzi wao upya chini ya umiliki wa Sir Jim Ratcliffe ukiendelea.

Mashetani Wekundu tayari imewaleta kikosini Joshua Zirkzee na Leny Yoro katika dirisha hili, huku gharama yao ya jumla ikiwa tayari inakaribia kufikia kiwango cha pauni milioni 100.

United inasemekana kutamani kuleta nyota wengine katika ubora wao ili kusaidia vipaji vyao vya vijana na pia kucheza pamoja na nyota wakongwe kama vile Bruno Fernandes na Casemiro. Kwa upande mwingine wa Manchester, City pia wanamfuatilia Olmo baada ya kukamilisha usajili wao wa kwanza wa majira ya joto hivi majuzi kwa kumnasa Mbrazil Savinho kutoka kwa Troyes.

Bayern Munich imekuwa na shughuli nyingi zaidi sokoni ikiwa na Michael Olise, Hiroki Ito na Joao Palhinha, lakini inataka mchezaji mwingine mbunifu ili kuimarisha safu ya kikosi hicho cha kocha Vincent Kompany. Olmo na Xavi Simons ndio chaguo mbili muhimu zinazozingatiwa Allianz Arena.



## Simba yakiri dili la Mpanzu gumu

INATOKA UK. 24

kila siku hakuna sehemu ambayo wanakosa kuliongelea," alisema mratibu huyo.

Simba itakwenda kucheza mechi yake ya tamasha la Simba Day dhidi ya APR ya Rwanda, Agosti 3, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Tamasha hili mwaka huu litafanyika kwa mara ya 16 tangu kuanzishwa kwake mwaka 2009 na aliyekuwa Mwenyekiti wa klabu hiyo kwa wakati huo, Mzee Hassan Dalali.

## Aziz Ki afichua

INATOKA UK. 24

bora msimu ujao utabaki kwetu, tuna Mzize, Musonda, halafu kuna Dube, yaani msimu ujao mfungaji bora atatokea tena Yanga," alisema.

Mchezaji huyo ambaye usajili wake kuelekea msimu ujao ulizua gumzo kubwa kwenye vyombo vya habari kutokana na kuonekana kutakiwa na klabu kadhaa za Afrika, alisema ana uhakika mashabiki wa Yanga watasafiri kwa wingi kueleka Burundi kama mechi yao ya awali Ligi ya Mabingwa Afrika itachezwa huko.

"Nina imani mashabiki wengi watajitokeza kwenda Burundi ili kutupa sapoti kwa sababu niliona msimu uliopita walivyojitokeza kwa wingi kwenda Rwanda katika mechi yetu dhidi ya Al Merrikh, timu hii ina mashabiki ambao ni kama familia moja, wako karibu sana na timu yao."

Msimu uliopita mashabiki wengi wa Yanga walisafiri mpaka Rwanda katika mechi yao ya raundi ya kwanza dhidi ya timu hiyo ya Sudan ambapo kwa kiasi kikubwa iliwasaidia kuibuka na ushindi wa mabao 2-0, Septemba 16 mwaka 2023 na kuweza kutinga hatua ya makundi.

El Merrikh ilishindwa kucheza kwenye ardhi yao kutokana na machafuko ya kisiasa.

Hata hivyo zipo habari kuwa Vital'O huenda isitumie uwanja wa nyumbani kwao kutokana na kutokidhi vigezo vya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF).



# TWIGA STARS WATAFANYA VIZURI WAFCON -TFF

**Na Shufaa Lyimo**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF) limesema ubingwa walioupata timu ya taifa ya wanawake 'Twiga Stars' kwenye michuano ya Tunisia (Tunis Womens Cup 2024) utawasaidia kufanya vizuri kwenye fainali za Afrika za wanawake 'WAFCON' zitakazofanyika mwaka huu nchini Morocco.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mara baada ya kikosi cha timu hiyo kuwasili kwenye Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Rais wa TFF, Wallace Karia aliipongeza timu hiyo kwa kufanya vizuri kwenye mashindano hayo na kupeperusha vema bendera ya Tanzania.

**"Mashindano haya yalikuwa sehemu ya maandalizi kuelekea kwenye mashindano ya WAFCON ambayo yatafanyika mwaka huu kwani malengo yetu ni kuona timu inakwenda kushindana na si kushiriki," alisema Karia.**

Aidha, alisema wameamua kuitumia michezo ya kirafiki ya kalenda ya FIFA ili benchi la ufundi la timu hiyo lihakikishe linaunda timu yenye ushindani kuelekea kwenye fainali hizoza Afrika.

Kwa upande wake, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime alisema amefurahishwa na viwango vilivyoonyeshwa na wachezaji wake katika mashindano hayo na kudai walikwenda kwa lengo la kutwaa kombe hilo.

Alisema kuelekea kwenye fainali za WAFCON, watakaa na kuzungumza na TFF kwa ajili ya kujadili mapungufu na changamoto zao kwa ajili ya kuhakikisha wanakwenda kufanya vema nchini Morocco.

"Tumefurahishwa na mafanikio haya ambayo tumetumia kalenda ya FIFA kwa kucheza michezo mfululizo itakayotusaidia kufanya vizuri kwenye WAFCON," alisema Shime.

Kwa upande wa wachezaji, nahodha wa timu hiyo, Anastazia Katunzi, alisema ushindi huo utawasaidia kuipeperusha vema bendera ya Tanzania na kuwataka watanzania waendelee kuwaamini kwa kuwa malengo yao ni kufika mbali.

Timu hiyo ilicheza michezo miwili mchezo wa kwanza walicheza na Botswana na kutoka Suluhu ya kutokufungana wakati mchezo wa pili iliichapa wenyeji, Tunisia mabao 5-0 na kutwaa ubingwa huo.



Vijana wa Kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa kituo hicho jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kocha Kitambi aiweka Singida BS kimataifa*

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA msaidizi wa klabu ya Singida Black Stars, Denis Kitambi, amesema usajili walioufanya na uwepo wa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Patrick Aussems anaamini timu hiyo itacheza michuano ya kimataifa msimu ujao.

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni kutoka mkoani Arusha ambako timu hiyo imeweka kambi yake kujiandaa na msimu ujao, alisema malengo yao msimu ujao ni kuhakikisha timu hiyo inapata nafasi ya kucheza mashindano ya kimataifa.

"Kwa wachezaji waliopo ndani ya timu hii tuna matumaini makubwa ya kushiriki mashindano ya Kimataifa msimu ujao mashabiki wategemee burudani kutoka kwetu, uwepo wa wachezaji wenye uwezo na benchi zuri la ufundi itatufikisha pale tunapotaka kufika," alisema Kitambi.

Aidha, alisema wachezaji wao wana viwango vya cha Kimataifa ambavyo vitaleta ushindani mkubwa msimu huo ambao unatarajiwa kuwa na upinzani mkubwa.

Alisema tangu ajiunge na timu hiyo wachezaji na viongozi wamempa ushirikiano mkubwa hali inayompa matumaini ya kutimiza malengo yao.

Kwa upande wake Ofisa Habari wa timu hiyo, Hussein Masanza akizungumzia hali ya kambi yao alisema kila kitu kinaenda vizuri huku morali yavwachezaji ikiwa juu.

Amewahaidi mashabiki kupata furaha kutokana na aina ya wachezaji waliowasajili msimu huu.

Michezo
Jumapili Julai 21, 2024
Nipashe



Olmo awa lulu Ulaya UKURASA 21

# Simba yakiri dili la Mpanzu gumu

## ●●● Yasema klabu yake ya AS Vita haitoi ushirikiano, lakini bado inapambana ili...

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa klabu ya Simba kwa mara ya kwanza umejitokeza hadharani na kukiri kuwa ilikuwa inamuwania kwa udi na uvumba winga wa AS Vita, Elie Mpanzu, lakini dili hilo limekuwa gumu ingawa bado inaendelea kupambana dakika hizi za mwisho za dirisha la usajili.

**Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema jana kuwa tatizo si pesa, bali klabu yake haitaki kumuachia, huku pia ikiwa hata haisemi thamani halisi ya mchezaji huyo.**

"Mpanzu dili lake limekuwa gumu, klabu yake imekuwa na changamoto sana, tatizo siyo pesa, ila inaonekana haipo tayari kumuachia, bahati mbaya ana mkataba nao na hata bei hawasemi, wangetuambia wanamuuza tungemnunua, kwa hiyo niwaambie wanachama na mashabiki wa Simba kwa sasa dili limekuwa gumu, siwezi kusema atapatikana au lah lakini tunaendelea kupambana, lolote linaweza kutokea, hata hivyo kama ikishindikana basi tutaendelea na tulionao kwa sababu tuna kikosi bora," alisema Ahmed.

Alisema hata hivyo bado wanaendelea kumfuatilia na ikishindikana dirisha hili hata dirisha lijalo watahakikisha wanakamilisha dili hilo.

Hii ni mara ya kwanza klabu hiyo kujitokeza hadharani kukiri kumuwania mchezaji huyo ambapo awali zilikuwa ni tetesi na hakukuwa na taarifa rasmi za kumuhitaji mchezaji huyo.

Wakati hayo yakiendelea, huko kambini nchini Misri, wachezaji wapya wa kigeni wa Simba wameonekana kulizungumzia zaidi tamasha la kila mwaka la klabu hiyo maarufu 'Simba Day'.

Mratibu wa klabu hiyo, Abbas Ally, akiwa Ismailia nchini Misri, amesema kwa sasa wachezaji wote wapya wa kigeni, wameonekana kuzungumzia tamasha hilo huku wengine wakiingiwa shauku kwani wanafahamu watakwenda kutambulishwa mbele ya umati wa mashabiki 60,000 huku baadhi yao ikiwa ni mara kwanza kushuhudia.

"Kiukweli kambini kila mchezaji mpya amekuwa na hamu sana ya kutaka kujua kuhusu Simba Day. Kama unavyofahamu ni tamasha kubwa sana kwa sasa Afrika, na imekuwa ni gumzo kubwa kwa hiyo kila mchezaji ana hamu ya kutaka kulishuhudia, pia wapo kwenye hofu kwa sababu wanaambiwa uwanja wa Benjamin Mkapa unaochukua mashabiki 60,000 unajaa wote, kwa hiyo katika mzungumzo ya

INAENDELEA UK. 23



# Aziz Ki afichua siri yake na Chama

**Na Mwandishi Wetu**

MSHINDI wa kiatu cha dhahabu katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita, Stephane Aziz Ki, amefichua siri baina yake na mchezaji mpya kwenye klabu hiyo, Clatous Chama kuwa kila mmoja alitaka kucheza timu moja na mwenzake.

Aziz Ki, ambaye msimu uliopita alikuwa mchezaji tegemeo kwenye kikosi hicho, akiibuka pia mfungaji bora wa Ligi Kuu kwa kupachika mabao 21, amesema kwa muda sasa kila mmoja alikuwa akimpongeza mwenzake anapofanya vema katika michezo mbalimbali na kutamani siku moja wakutane kwenye timu moja.

"Chama ni mchezaji mzuri sana, tangu yupo Simba alikuwa akinikubali, akinipa pongezi mara kwa mara na kusema anataka kucheza timu moja na mimi, hata mimi mwenyewe kutokana na kuona jinsi alivyokuwa akifanya akiwa na kikosi chake nilitamani pia siku moja kucheza naye na ndoto hii hatimaye imetimia, tuko wote Yanga," alisema Aziz Ki.

Kuhusu ufungaji bora msimu ujao, kiungo mshambuliaji huyo anayechezea pia timu ya taifa ya Burkina Faso, ametabiri kiatu cha dhahabu msimu ujao kitabaki Yanga, akiwataja wachezaji Kennedy Musonda, Clement Mzize au Prince Dube mmoja wao ni lazima akivae.

"Nadhani msimu huu tutakwenda mbali zaidi kwa sababu tumesajili wachezaji wazuri sana, nina imani kikosi chetu kitakuwa tishio zaidi.

"Kikosi bado kina Pacome, Maxi na sasa kimeongezewa uwezo wa Chama na Prince Dube, kusema kweli kiko imara na tunaweza kufanya makubwa zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, nadhani hata ufungaji

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >